# Nipashe

Jumanne Novemba 10, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580395

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




**SABABU** zilizotuliza mfumuko wa bei

UKURASA 4



**SIMU** ilivyosaidia kunasa mwizi wa gari

UKURASA 4

**Zidane akubali kubeba lawama kipigo Madrid**

UKURASA 20

# Nani kubaki, kuachwa Baraza la Mawaziri

• **JPM** aweka wazi msimamo, awapa neno wateule wake, ampa majukumu AG... *Endelea ukurasa 2*



Rais John Magufuli akimwapisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, Ikulu Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**RAIS KULIZINDUA BUNGE WIKI HII**

WAKATI Bunge la 12 likianza mkutano wake wa kwanza leo, Rais Dk. John Magufuli anatarajiwa...

UKURASA WA 8

**MVUA YAUA WAWILI, 3 WAJERUHIWA**

WATU wawili wamepoteza maisha katika Manispaa ya Kigoma Ujiji na wengine watatu...

## Lema na Nyalandu matatani

UKURASA 8



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, hafla hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Diwani mteule CCM, wajukuu wafariki kwa kuteketea moto



UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



SALAMU ZA PONGEZI



Gazeti Nipashe linampongeza Rais Dkt John Magufuli na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha Miaka 5. 2020 - 2025

Kwa salamu za pongezi
Wasiliana nasi kwa Simu: 0686 101335
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



SALAMU ZA PONGEZI

# Nani kuachwa, kubaki Baraza la Mawaziri

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amedokeza kuwapo kwa mabadiliko katika baraza lake la mawaziri na kusema kuna watakaorudi na watakaoachwa.

Pia, amewatoa hofu wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kwa kuwahakikishia kuwa inawezekana kusiwe na mabadiliko kwa ambao wanachapa kazi, isipokuwa kwa watakaostaafu au kufanya vinginevyo.

Akizungumza baada ya kumwapisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Adelardus Kilangi, Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma jana, alisema mara kwa mara anapokea ujumbe mfupi wa maandishi kutoka kwa viongozi hao.

"Pamekuwa na tabia kila serikali mpya au awamu mpya inapoingia watu wanakuwa na hofu hasa watendaji wa serikali, kwamba panatokea mabadiliko, kwa sasa ninaona wana hofu sana wakuu wa mikoa na wilaya na ninawashangaa kwanini wanakuwa na hofu," alihoji.

"Kama ni mafanikio ya serikali ni pamoja na wao, kama ni ushindi wa asilimia 84 ni pamoja na wao wamewezesha kupatikana kwa kufanya kazi nzuri katika maeneo yao," alisema.

"Wanasiasa ambao tumeguswa na hili ni mimi (rais) ambaye ilibidi nikaombe kura kwa miaka mitano, pamoja na makamu wangu, waziri mkuu kwa sababu lazima tuteue waziri mkuu, mawaziri, spika na naibu spika ambao lazima wapigiwe kura," alisema na kuongeza:

"Mkuu wa mkoa unakuwa na wasiwasi gani, labda utendaji wako haukuwa mzuri, nashangaa napata ujumbe mfupi wa maandishi Mh. Rais nimejitahidi katika kipindi changu, kana kwamba nilimwambia kipindi chake kinaisha baada ya mimi kuapishwa," alisema.

"Nimeona nilizungumze kwamba Ma- RC na Ma -DC msiwe na wasiwasi na inawezekana pasitokee mabadiliko labda kwa atakayestaafu au kufanya mambo ya ovyo sana, kwanini nibadilishe RC, DC, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au Katibu Tawala Mkoa na Wilaya, serikali ni ile ile."

"Kama nilikuteua miaka miwili au mitano iliyopita si uwezo ni ule ule na mtu ni yule yule, wachape kazi wasipochapa kazi shauri yao, wakijindaa wanaondoka basi, nilianza nao nitamaliza nao, hii ni kwa watendaji wote makatibu wakuu, vyombo vya ulinzi na usalama...Katibu Mkuu Kiongozi nanyi mtakuwa ni nyie nyie," alisema.

"Natoa wito kwa watendaji wenzangu ndani ya serikali watu wachape kazi, kuchaguliwa kwetu hakuna maana tumekuja kubadilisha, hakuna mabadiliko tulianza wote na tutamaliza wote," alisema.

**MAWAZIRI**

"Mabadiliko yatakayokuwapo ni kwenye nafasi za uwaziri ambazo tulienda kuomba kura wote, hizo lazima tutabadilisha, wapo watakaorudi, wapo ambao hawatarudi tena siku hizo zipo 'option' (chaguo) ni kubwa nina wabunge 264 kwa hiyo uchaguzi ni mkubwa zaidi sitaki kusema uongo, nikishamaliza hivyo basi wengine wachape kazi tu," alisema.

"Watendaji wa serikali chapeni kazi, mpo na mtaendelea kuwapo labda ikifika muda wa kustaafu hilo ni suala jingine, au umeamua mwenyewe kuacha, au utendaji hauendani na kasi yetu, nionavyo kwa sasa kila mtendaji kila mahali wachape kazi, hakuna cha kuwa na wasiawasi, yaani kila mwaka unaapisha, hata kuapisha kunachosha," alisema.

**UJUMBE KWA AG**

"Watanzania wasingependa kuona kesi za serikali zinashindwa wakati mwanasheria wa serikali yupo, ni mwanataaluma na amefanyakazi kwenye Jumuiya za kimataifa, Watanzania maskini watapenda waone kesi zinazopelekwa mahakamani zinazohusu serikali na mali zao, zitetewe kwa haraka na kupata ufumbuzi mapema," alisema.

"Ukajipange kweli kweli, usimamie vizuri ofisi yako ili yanayohusu maslahi makubwa ya Watanzania ukayashughulikie kikamilifu, kazi ni dhamana na dhamana hii tumekupa kwa niaba ya Watanzania, kipindi cha kwanza ulifanya kazi zako vizuri ndiyo maana tumekuona tena," alisema.

Alisema pamekuwa na tabia kila serikali mpya au awamu nyingine inapoingia watu wanakuwa na hofu.

**MWANASHERIA MKUU**

Awali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Prof. Kilangi, alisema ameanza majukumu hayo akiwa na uelewa mkubwa na namna ya kukabiliana na mambo mbalimbali.

"Kazi kubwa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali siyo kuwa mtaalamu na mahiri katika sheria, bali kufahamu muktadha na mazingira ambayo sheria hiyo itatumika, sheria haitumiki hewani...dhana ya mapambano ya kisheria ambayo hutokea kutokana na changamoto au mikingamo inayoweza kujitokeza katika utendaji kazi," akimnukuu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Marekani, Erick Hollder.

Alisema ameiona nia ya serikali kuleta maendeleo kwa watu na kwa haraka, kupunguza utegemezi na hakujua kama ukitangaza nia ya kulinda rasilimali unatangaza vita inayoibua mapambano ya kisheria, ambayo hupiganwa ndani na nje, na kuahidi kufanya kazi kwa bidii.

**JAJI MKUU**

Naye, Jaji Mkuu wa Tanzania, Ibrahimu Juma, alimtaka Mwanasheria Mkuu kusoma andiko la Kamisheni ya Umoja wa Haki za Binadamu linalozungumzia kuwa sheria zinafanyakazi kwa manufaa ya wote, ambalo ni muhimu katika kutekeleza majukumu ya kisheria.

"Hakikisha sheria inawasaidia, inawawezesha maskini ambao ndiyo wengi, wengi huachwa katika tafsiri za kisheria," alisema.

## Cheyo alilia kupata ruzuku

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Chama cha United Democratic Party (UDP), John Cheyo, amesema ni wakati mwafaka kwa Chama Cha Mapinduzi ( CCM) chenye wawakilishi wengi bungeni, kuona umuhimu wa kupeleka bungeni muswada wa marekebisho ya sheria ya ruzuku ili kuviepusha vyama vya siasa kuwa ombaomba.

Cheyo, ambaye ni mwenyekiti tangu mwaka 1992 UDP ilipoanzishwa na kupata usajili, alisema kitendo cha vyama vya siasa kuwa ombaomba sehemu nyingine ni hatari kwa taifa.

Cheyo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Katika mkutano huo, kiongozi huyo ambaye mchakato wa uchaguzi mkuu chama chake kilimuunga mkono kwa asilimia 100 Rais John Magufuli kwa kutomsimamisha mgombea kwenye nafasi hiyo, alisema vyama vya siasa vilivyo vingi havina njia ya kupata mapato ya kujiendesha ikiwa ni pamoja na kulipa pango.

"Tunaamini muswada huu ukipelekwa bungeni na kwa sababu Chama Cha Mapinduzi kina wawakilishi wengi, waupitishe ili vyama hivi viendelee kuwapo," alisema.

Haya hivyo, Cheyo alisema pamoja na kwamba CCM ina wawakilishi wengi bungeni haimaanishi kwamba mfumo wa vyama vingi ndiyo umekufa. Alisema anaamini Rais Magufuli atatafuta njia ya kuvisaidia vyama vya siasa ili viendelee kuishi.

Kwa mujibu wa sheria ya ruzuku, vyama vyenye uwakilishi bungeni ndivyo vinavyostahili kupata ruzuku. Hata hivyo, UPD haina uwakilishi.

Cheyo aliwataka wanasiasa wenzake kujiepusha na kauli zinazoashiria uvunjifu wa sheria.

Pia alisema kwa viongozi wa vyama vya siasa waliojitokeza wakati wa kuapishwa kwa marais, wameonyesha ukomavu wa kisiasa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Theobald Sabi, akifuatilia kwa makini majaribio ya kisayansi kutoka kwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ghome yakiongozwa na mwanafunzi Emmanuel Abeli (katikati) wakati wa mahafali ya 11 ya shule hiyo. Kulia kwake Mkurugenzi wa Shule hiyo, Dk. Emmanuel Malangalila. **PICHA: IKULU**

# ...Kulizindua rasmi Bunge wiki hii

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAKATI Bunge la 12 likianza mkutano wake wa kwanza leo, Rais Dk. John Magufuli anatarajiwa kuzindua rasmi na kuhutubia Taifa wiki hii jijini Dodoma.

Aidha, kiapo cha wabunge wote kitaanza leo hadi Novemba 12, mwaka huu.

Bunge hilo litaketi kwa siku nne kutekeleza majukumu sita ambayo ni kusomwa kwa tangazo la Rais kuitisha Bunge, uchaguzi wa Spika, kiapo cha uaminifu kwa wabunge wote, kuthibitisha jina la Waziri Mkuu, uchaguzi wa Naibu Spika na ufunguzi rasmi wa bunge hilo jipya.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliyasema hayo jana baada ya kupokea msaada wa mabegi 400 ya wabunge yenye thamani ya Sh. milioni 100 yaliyotolewa na Benki ya CRDB.

"Mheshimiwa Rais siku ya Alhamisi jioni au Ijumaa asubuhi atakuwa anahutubia Taifa kupitia bunge, inaanzisha awamu hii ya pili ya awamu ya tano ya serikali anayokwenda kuiunda," alisema.

Kuhusu benki hiyo, Spika Ndugai alishukuru kwa msaada huo huku akiiomba benki hiyo kupunguza riba kwenye mikopo ili kutoa unafuu kwa wabunge na Watanzania.

"Kwa kuwa wabunge wana ushawishi mkubwa kwa wapigakura na mabalozi wakubwa, mziangalie riba zenu kuwe na 'special rate' inayotoa unafuu wa maisha kwa wabunge na watanzania kwa ujumla," alisema.

Alieleza kuwa riba ikipungua inatoa unafuu mbalimbali hasa kwa wafanyabiashara, wafanyakazi ili kurejesha kwa unafuu mkubwa.

"Wabunge watafurahi mabegi haya ni ya kiwango cha juu sana, yatasaidia kuweka nyaraka mbalimbali ikiwamo tablet nia ni kurahisisha utendaji wa mbunge, siku hizi bunge letu ni la kisasa hatuhitaji manyaraka makubwa tunaendesha bunge mtandao kikubwa ni tablet," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, alisema benki hiyo ina mahusiano mazuri na bunge hilo na wamekuwa wakishirikiana na wabunge kwa mambo mengi.

"Benki yetu tunajali sana mahusiano, wabunge wanapokuwa bungeni nyaraka ni nyingi, benki iliona ni vyema kuandaa mabegi rasmi ambayo yana hadhi ya wabunge yapo 400, tunaimani mabegi yanaweza kuhifadhi mambo yote hayo na kutembea vizuri," alisema.

Katika hatua nyingine, Ofisi ya Bunge iliwataka wabunge wateule kila mmoja kuambatana na wageni wasiozidi 20 wakati wa uapisho.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 09-11-2020

**TANGAZO**

Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATANO tarehe 11-11-2020 kampuni ya **YOHANA ANTHONI SENGASU** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea MBEYA kupitia VIGWAZA.

Gari hilo lenye namba za usajili zenye vipimo vyake:

1) T 935 DQS / T 386 CHR
UREFU 23 UPANA 4.4
KIMO 5.2

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza

## HABARI KITAIFA

# Diwani mteule CCM, wajukuu wafariki kwa kuteketea moto

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

DIWANI mteule wa Kata ya Kikongo, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Fatuma Ngozi na wajukuu zake wawili, wamefariki dunia baada ya nyumba waliyokuwa wakiishi kuteketea kwa moto usiku wa kumkia Novemba 9.

Taarifa kutoka eneo la tukio zimedai kuwa tukio la kuungua moto nyumba hiyo lilitokea usiku wa saa nane Ngozi akiwa amelala na wanafamilia, watoto na wajukuu.

Baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo walisema, moto huo ulianza kuzuka katika chumba cha diwani huyo na baadaye kusambaa nyumba nzima jambo ambalo lilizua taharuki na hivyo kushindwa kuzimwa kwa haraka.

Imedaiwa kuwa Ngozi na mjukuu wake mmoja Haji Hamisi, mwenye umri wa miezi saba, walikutwa wamefariki papohapo kutokana na kuungua vibaya na majeruhi watano walifikishwa katika Hospitali ya Tumbi wakiwa na hali mbaya, huku mjukuu mwingine aliyejulikana kwa jina la Fatuma, alifariki muda mfupi baada ya kufikishwa hospitalini hapo.

Pia, majeruhi wanne ambao ni Ashura Ramadhani, Rehema Ramadhani, Abrahaman Selemani na Monica ambaye alikuwa mfanyakazi wa ndani, wamepelekwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa matibabu zaidi.

Mbunge mteule wa Jimbo la Kibaha Vijijini Michael Mwakamo (CCM), amekiri kupata taarifa ya kifo cha diwani huyo na kwamba ameacha pengo katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Kibaha Vijijini.

Mwakamo, alisema alipata taarifa usiku saa nane akiwa Dodoma alipokwenda juzi kufanya maandalizi ya shughuli za kuapishwa, lakini alilazimika kurudi kushiriki katika msiba huo.

Diwani mteule wa viti maalum Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Vijijini, Josephine Gunda (CCM), alisema alipata taarifa hiyo saa nane kasoro usiku.

Alisema, baada ya kupata taarifa hiyo alimpigia simu mbunge mteule wa jimbo hilo, Michael Mwakamo, ili aweze kufanya mawasiliano na watu wa kituo cha afya kwa ajili ya msaada wa kupeleka gari eneo la tukio.

Gunda, alisema alipofika katika eneo la tukio alikuta tayari nyumba imeteketea yote huku miili ya marehemu ikiwa inatolewa nje kwa ajili ya kupelekwa chumba cha kuhifadhia maiti kituo cha afya Mlandizi.

Alisema, kuwa majeruhi waliopelekwa kituoni walihamishiwa Hospitali ya Tumbi, Kibaha mkoani Pwani na baadaye Hospitali ya Rufani ya Taifa Muhimbili.

Katibu wa CCM Kibaha Vijijini, Rukia Mbasha, alieleza kusikitishwa na tukio hilo huku akiomba vyombo vya usalama vifanyekazi yake ili kubaini chanzo halisi cha moto huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba uchunguzi zaidi unaendelea kubaini chanzo cha moto huo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Rufani Tumbi, Edward Wayi, alithibitisha kupokea majeruhi watano waliokuwa wameungua moto mwili mzima, kati yao mmoja alifariki akiwa hospitalini na wengine wawili kukimbizwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa matibabu zaidi.

# CHADEMA yakana kupeleka majina viti maalum

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema hakijawasilisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), majina ya wabunge wateule wa viti maalum kama taratibu zinavyoelekeza.

Taarifa ya Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya CHADEMA, Tumaini Makene, ilinukuu barua ya Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, ya Novemba 9, mwaka huu, yenye kumbukumbu namba C/HQADM/20/TU/05/140.

Barua hiyo ilitoka kwa Katibu Mkuu huyo kwenda kwa Mkurugenzi wa NEC, kuwa Kamati Kuu ya CHADEMA hadi sasa haijafanya uteuzi wowote na nafasi za viti maalum wala kuwasilisha majina Tume.

"Katibu Mkuu ndiye mwenye mamlaka ya kuwasilisha orodha ya majina ya wanaopendeezwa kuteuliwa kuwa wabunge haijawasilishwa ordha yoyote," alisema.

Aidha, taarifa hiyo ilidai kuwa Mnyika alizungumza kwa simu na Mwenyekiti na Mkurugenzi wa NEC, Novemba 7 na 8, mwaka huu, kumtaarifa kuwa CHADEMA hakijafanya uteuzi wala kuwasilisha majina ya wanaopendekezwa.

"Ikumbukwe Novemba 9, mwaka huu, NEC ilileta barua yenye Kumb.Na EA75/162/08B/75 saa tisa jioni ambayo ilitaka fomu na orodha ya wabunge na madiwani wa Viti Maalum viwasilishwe kabla ya Novemba 7, mwaka huu," alisema Makene.

Juzi Mkurugenzi wa NEC alikaririwa akisema kuwa idadi ya Viti Maalum kwa CCM ni 94 na CHADEMA wana 19.

# Mgombea ubunge, wafuasi kortini

**Na Said Hamdani, LINDI**

WATU 11 akiwamo aliyekuwa mgombea Ubunge Jimbo la Nachingwea mkoani Lindi, kupitia tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamefikishwa mahakamani, wakidaiwa kukutwa na vifaa hatarishi kinyume cha Sheria ya Usalama wa Taifa.

Waliofikishwa katika mahakama hiyo ya Mkoa wa Lindi, ni Mahadhi Mmoto (37), aliyekuwa mgombea ubunge wa Jimbo la Nachingwea, Ahmadi Issa Bilali (35), Ramadhanai Mohamedi Chikawe (32), Fadhili Slimu Akremi (30), Rashidi Saidi Kamutu (26) na Martin David Kamonga (31).

Wengine ni Michael Makoe Mpima (25), Salum Juma Jabu (50), Ally Salum Lihomange (28), Salum Mohamedi Pahi (40) na Shabani Selevester Nkane (28). Hata hivyo miongoni mwa washtakiwa hao watatu wamefikishwa mahakamani hapo wakiwa wamevunjwa miguu na kulazimika kupewa msaada wa kubebwa pale walipokuwa wakishushwa kwenye gari na pale chooni.

Mwanasheria wa Serikali, Abdurahamani Mohamedi, alidai washtakiwa hao wamefanya kosa hilo ka kukutwa na vifaa hatarishi Oktoba 28, mwaka huu usiku, mtaa wa Boma mjini Nachingwea. Alivitaja vifaa hivyo hatarishi ni pamoja na lita 40 za petroli, maski za kuficha uso mbili pamoja na mapanga ambayo hata hivyo haikutajwa idadi yake.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

(**Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ("Muombaji") kwa ajili ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Dar es Salaam, miji ya Kibaha, Bagamoyo, Mkuranga, Kisarawe na Chalinze katika Mkoa wa Pwani pamoja na vijiji katika sehemu za Halmashauri ya Wilaya za Bagamoyo, Kibaha na Morogoro Vijijini.

EWURA inakaribisha maoni kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Muombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:-

| |
|---|
| **1: Jina na Anuani:** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA),<br>DUNGA /MALANGA RD, MWANANYAMALA,<br>S.L. P 1573<br>Dar es Salaam,<br>Tanzania.<br>Barua Pepe: info@dawasa.go.tz<br><br>Tovuti: www.dawasa.go.tz<br>Simu : +255 22 27600015<br>: 0800110064 |
| **2: Maelezo ya Leseni:** |
| Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Dar es Salaam, miji ambayo ni ya Kibaha, Bagamoyo, Mkuranga, Kisarawe na Chalinze katika Mkoa wa Pwani pamoja na vijiji katika sehemu za Halmashauri ya Wilaya za Bagamoyo, Kibaha na Morogoro Vijijini. |
| **3: Vyanzo vya Maji na Miundombinu** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ina vyanzo vikuu vya maji vya aina mbili ambavyo ni maji ya visima na maji ya mito. DAWASA ina jumla ya visima 56 ambavyo vina uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 19,203 kwa siku na vyanzo vikuu vinne vinavyotegemea maji ya mto (Ruvu Chini, Ruvu Juu, Mtoni na Wami) vyenye uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za ujazo 482,200 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji ya muombaji inajumuisha; matenki ya maji 159 yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo153,649. Muombaji pia ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 3,866; vilula 1,150 na mtandao wa majitaka wenye jumla ya urefu wa kilomita 201. Vilevile, muombaji ana mabwawa ya kutibu majitaka yaliyoko katika maeneo ya Ukonga, Mikocheni, Vingunguti, Buguruni, Airwing, Lugalo, Kurasini na Mabibo jijini Dar es Salaam. |
| **4: Umiliki** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. |

!

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030; Barua pepe: info@ewura.go.tz**
**Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

## Sababu mfumuko wa bei kubakia asilimia 3.1

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka uliishia mwezi Oktoba, 2020 umebaki kuwa asilimia 3.1 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia Septemba, 2020.

Mkurugenzi wa Sensa na Takwimu za Jamii ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ruth Minja, alibainisha hayo jana jijini Dodoma, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Minja alisema kuwa hali hiyo inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia Oktoba, 2020 imebaki kuwa sawa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2020.

"Mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba, 2020 kuwa sawa na mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba, 2020 umechangiwa na kupungua na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia mwezi Oktoba, 2020 zikilinganishwa na bei za mwezi Oktoba, 2019," alisema Minja.

Pia, alisema baadhi ya bidhaa za vyakula zilizopungua bei kwa mwezi Oktoba, 2020 zikilinganishwa na bei za mwezi Oktoba 2019 ni pamoja na mchele kwa asilimia 4.2, mahindi kwa asilimia 12.4, unga wa mahindi kwa asilimia 3.2, unga wa ngano kwa asailimia 0.9.

Aliongeza kuwa, bidhaa zingine ni unga wa mtama kwa asilimia 0.8, unga wa muhogo kwa asailimia 1.4, mihogo mibichi kwa asilimia 2.5, viazi vitamu kwa asilimia 5.4 na ndizi za kupika kwa asilimia 6.3.

# Simu yafanikisha mwizi wa gari kufungwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi, imemhukumu mkazi wa Yombo, jijini Dar es Salaam, Bakari Msanga (25), kifungo cha miaka minne jela kwa kosa la wizi wa gari.

Gari hilo lenye thamani ya Sh. 14,600,000 ni mali ya mtumishi wa Shirika la Umeme Nchini (TANESCO).

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Elimo Masawe, baada ya mshtakiwa kukiri kosa.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo na Mwanasheria wa Serikali, Emmanuel John, kuwa Oktoba 26, mwaka jana, mshtakiwa alienda nyumbani kwa Priscus Mahango na kuiba gari aina ya Toyota, namba za usajili T897 DNH lenye thamani ya Sh. milioni 14.6 na kutokomea nalo.

John alidai kuwa kukamatwa kwa mshtakiwa kumefanikishwa na simu ya mkononi ambayo mlalamikaji aliisahau kwenye gari na mshtakiwa huyo alipoiona aliichukua na kumpa mpenzi wake wa kike.

Mwanasheria huyo wa serikali, alidai kuwa baada ya mlalamikaji kugundua simu yake moja aliisahau kwenye gari lake lililoibwa, waliipiga na kupokewa na mwanamke huyo ambaye alipofuatiliwa alikamatwa eneo la Yombo, jijini Dar es Salaam na kufanikisha kumwonyesha mshtakiwa alipo.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea na kuiomba mahakama kutompatia adhabu kali kwa madai kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza na ana familia wakiwamo wazazi wanaomtegemea.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, John, aliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia kama hiyo.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Massawe, alisema anamhukumu mshtakiwa kifungo cha miaka minne gerezani na kulipa fedha ya thamani ya gari aliloiba.

Hata hivyo, gari hilo halijapatikana na vyombo vya dola vinaendelea kulitafuta liweze kukabidhiwa kwa mmiliki.




Mbunge mteule wa Kongwa, Job Ndugai (wa pili kulia), akikabidhiwa moja ya mabegi 400 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), kwa niaba ya wabunge wote ambao watakabidhiwa mabegi hayo. Sherehe ya makabidhiano ilifanyika katika ofisi za Bunge jijini Dodoma jana. Kulia ni Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Mwambapa (kushoto). **PICHA: BUNGE**


NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

M/MWANZO YA ILEMELA - SHAURI LA MADAI Na. 106/2017
HAPPIFANIA LINUS ______ MDAI
DHIDI YA
ANDREA YAKOBO BULALO ______ MDAIWA

M/MWANZO YA MKUYUNI - SHAURI LA MADAI Na. 37/2020
REBECA AYUBU ______ MDAI
DHIDI YA
PASCHAL SILVESTER ______ MDAIWA

M/MWANZO YA MJINI - SHAURI LA MADAI Na. 43/2020
YASINTA NELIWA KOLOSPERU ______ MDAI
DHIDI YA
FELIX MWESIGA ______ MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO YA MKUYUNI, MAHAKAMA YA ILEMELA NA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WANANDOA AMBAZO NI NYUMBA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | BOMA LA NYUMBA | MTAA WA KUZENZA-NYEGEZI | 10/12/2020 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | NYUMBA | MTAA WA MKUDI-GHANA NYUMBA NAMBA 001/057 | 10/12/2020 SAA 8 MCHANA NA KUENDELEA |
| 3 | NYUMBA | IGOMA BLOCK C NA 6 | 11/12/2020 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |

MASHARTI YA MNADA:
1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

MAWASILIANO: 0768-588155/0782-405140


# Athari mgongano binadamu, wanyamapori zawekwa wazi

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imesema zaidi ya watu 50 wamekuwa wakipoteza maisha kila mwaka na karibu heka zaidi ya 5,000 huharibiwa nchini kutokana na mgongano wa binadamu na wanyamapori kwenye maeneo ya hifadhi yanayozungukwa na wananchi.

Kaimu Kamishna wa Uhifadhi TAWA, Mabula Nyanda, alisema hayo jana wakati akifungua kikao cha menejimenti ya TAWA makao makuu na wakuu wa vituo vya hifadhi kilichofanyika mjini hapa, ambapo alisema suala la wanyamapori kuua au kuharibu mazao ya wananchi ni kubwa kwa sasa, hivyo TAWA imeona umuhimu wa kutoa elimu kwa wananchi hao.

Alisema wameshaandaa mpango mkakati wa udhibiti wa wanyama wakali na waharibifu, huku ikijipanga kutoa elimu kwa wakazi wa maeneo ya pembezoni mwa hifadhi, ili wasijikute wanapata madhara makubwa ikiwamo kuuawa.

Alisema watatao elimu kwa wananchi hao ikiwamo jinsi gani wajiepushe na wanyama hao kama tembo na simba, ambao mara nyingi wamekuwa wakiripotiwa kuleta mgongano kati yao na binadamu.

Alisema tembo wamekuwa wakiua binadamu kutokana na binadamu kutojua namna ya kuishi nao, kwa kufanya mambo mbalimbali ikiwamo kulima mazao rafiki kwa wanyama hao kama matikiti maji, kuwafuata na kupiga kelele wanapowaona.

Hivyo alisema wamejipanga kimkakati kuwafanya wananchi watumie mbinu mbalimbali za kujilinda ikiwamo kuhakikisha kazi zao hazihamasishi wanyama kuingia.

Alisema TAWA imejipanga kukabiliana na masuala ya rushwa huku ikianza na kuwawajibisha wakuu wa vituo vya uhifadhi wasiotoa taarifa za changamoto hizo mapema.

Naye Kaimu Kamishna msaidizi wa Kanda ya Kusini Mashariki, Henock Msocha, alisema watahakikisha wanaongeza ushirikiano katika kukomesha suala la ujangili sambamba na kutumia vyema elimu wanayopewa kwenye kikao hicho ili kudhibiti tatizo hilo.

# HABARI KITAIFA

## Watumishi wa elimu kunolewa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inakusudia kuendelea na mpango wa kutoa mafunzo kwa kada za elimu kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi kwa watumishi wa idara zilizopo chini ya wizara hiyo.

Imesema lengo la kutoa mbinu mpya ya kukabiliana na changamoto sehemu za kazi.

Hayo yalibainishwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo, mjini Morogoro wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa kada ya wahasibu, maofisa ugavi na manunuzi pamoja na wakutubi kutoka wizara hiyo.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA).

Dk. Akwilapo alisema mafunzo ni fursa nzuri kwa watumishi katika wizara hiyo, ili kupata mbinu mpya itakayowawezesha kuacha kufanya kazi kwa mazoea na badala yake kwenda na wakati.

"Mafunzo hayo ni muhimu kwa kada hiyo ya manunuzi na wahasibu ili kuwasaidia kupata mbinu mpya zitakazosaidia kuona fedha za serikali zinatumika vizuri," alisema Dk. Akwilapo.

Naye Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa wizara hiyo, Moshi Kabangwe, alisema mafunzo hayo ni mwendelezo kwa mwaka wa fedha uliopita kwa kada ambazo hazikushiriki kwenye mafunzo kutokana na sababu mbalimbali.

Kabangwe alisema mafunzo hayo yalilenga kujenga uwezo kwa watumishi hao kwenye msauala ya usimamizi wa fedha ili kuonyesha dhamani ya fedha ya serikali inaonekana.

Mratibu wa mafunzo hayo na mkufunzi mkuu kutoka TIA, Dk. Hassanal Mwakyoma, alisema mafunzo hayo yatawapa fursa watumishi wa umma kujua haki na wajibu wao wanapokuwa sehemu zao za kazi.

## Watafiti waelekezwa magonjwa yasiyoambukiza

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imezitaka taasisi za afya na watafiti kuwekeza katika kufanya utafiti wa kisayansi zitakazowezesha wananchi kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza ambayo yanatajwa kuongezeka kwa kasi nchini na kusababisha vifo.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Abel Makubi, akisoma hotuba ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Mabula Mchembe, kwa niaba yake katika ufunguzi wa kongamano la pili la kisayansi la maadhimisho ya Wiki ya Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza alisema yamekuwa yakiathiri kila mtu na wengine wamepoteza maisha.

Kongamano hilo limebebwa na kauli mbiu isemayo, 'Kuimarisha mifumo ya afya ili kuzuia magonjwa yasiyoambukiza' ambapo utafiti zaidi ya 200 ziliwasilishwa kwa njia ya maongezi na mabango.

Prof. Mchembe alisema magonjwa hayo yamesababisha hasara kubwa kwa taifa kwa kuondoa nguvu kazi na kurudisha nyuma maendeleo ya familia.

"Yanasababisha utegemezi sugu na wanaougua kushindwa kujihudumia na kuongeza mzigo kwa mfumo wa afya katika kuwahudumia kutokana na wengi hukaa hospitali muda mrefu," alisema.

Prof. Mchembe alisema takwimu za kitaifa za mwaka 2017 zinaonyesha magonjwa hayo yanachangia asilimia 33 ya vifo vyote ambapo vikivyoripotiwa kipindi hicho vilikuwa ni 134,600.

"Vifo hivyo vimetokana zaidi na magonjwa ya moyo na shinikizo la damu kwa asilimia 13, kisukari asilimia 2, saratani asilimia 7, na ajali asilimia 11," alisema.

Alisema hali hiyo haikubaliki na inawafanya wajumuike katika kujitathmini na kupanga mikakati ya pamoja ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Hata hivyo, alisema huduma za uchunguzi zimeboreshwa ikiwa ni pamoja na kuweka vifaa vya kisasa.

"Tunawapongeza kwa kufanya utafiti mbalimbali na wito wetu kwenu mjielekeze zaidi kufanya utafiti utakaotoa mbinu mpya za matibabu ya magonjwa haya ili kusaidia kutatua matatizo ya utoaji wa huduma," alisema.

Alisema wanahitaji majibu ya changamoto zilizopo Tanzania zinazotokana na utafiti wa ndani na kutumia zilizotolewa na nchi nyingine kwa kuziboresha.

"Dawa za tiba asili ambazo zinatibu magonjwa mbalimbali mfano shinikizo la damu na mzifanyie utafiti ili kuiwezesha nchi kugundua dawa.

"Tunapenda kupata mapendekezo yenu yanayotekelezeka na yaweze kuwafikia wadau wote ili kuwasaidia kutekeleza mipango yao."

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sayansi Shirikishi Muhimbili(MUHAS), anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri, Prof. Appolinary Kamuhabwa, alisema lengo la kongamano hilo ni kushirikishana na kuelekezana kuhusiana na utafiti mbalimbali zilizofanyika.

Alisema watashirikishana matokeo yake ili kuthibiti magonjwa yasiyoambukiza.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Huduma za Tiba kutoka Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe, alisema kwa takriban miaka nane magonjwa yasiyoambukiza yameongezeka na idadi ya vifo navyo vinaongezeka.

Alisema kila mwaka kwa wiki moja kuanzia Novemba 7, watakuwa wanaadhimisha maadhimisho hayo, ili kuongeza uelewa kwa wananchi wa namna ya kujikinga kupitia uzoefu wa utafiti mbalimbali zilizokwisha kufanyika.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo cha MUHAS, Prof. Andrea Pembe, alisema magonjwa yasiyoambukiza yamekuwa tishio ya kuathiri nguvu kazi ya taifa na kuongeza mzigo kwa serikali kuhusu matumizi ya rasilimali watu.

Alisema kongamano hilo limeandaliwa na chuo hicho chenye moja ya jukumu la kuandaa utafiti ambao unasambazwa kwa lugha rahisi yenye kueleweka.


CHAMA CHA WALIMU TANZANIA
CWT
WAJIBU NA HAKI

**CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)**

Chama cha Walimu Tanzania (CWT), kinapenda kutangaza mabadiliko ya ukumbi wa walimu walioitwa kwenye usaili wa nafasi ya Katibu wa Wilaya uliotarajiwa kufanyika tarehe 11 Novemba 2020 jijini Dodoma katika ukumbi wa LAPF na sasa usaili huo utafanyika katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kituo cha Dodoma tarehe 11 Novemba 2020 kuanzia saa 2 kamili asubuhi.

Ukiona tangazo hili mjulishe na mwenzio

Imetolewa na:

Mwl. Deus G. Seif
KATIBU MKUU – CWT.
09/11/2020



Bank of Baroda (Tanzania) Ltd.

**PONGEZI**



**Bodi ya Wakurugenzi, Uongozi na wafanyakazi wa Bank of Baroda (Tanzania) Ltd, wanaungana na Watanzania wote kuwapongeza Mh. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Mh. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa Miaka mitano tena kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .**

Bank of Baroda (Tanzania) Ltd,Plot No.149/32
Ohio/Sukoine Drive P. O. Box No. 5356, Dar es Salaam

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanafunzi elimu ya juu waharakishiwe mikopo

**KUANZIA** wiki hii vyuo vingi vya elimu ya juu vitafunguliwa, huku wanafunzi wakisubiri kupatiwa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya ya Elimu ya JUU (HESLB).

Wanafunzi ambao ni wahitaji wa mikopo kitu muhimu kwao ni kupatiwa mikopo hiyo ili waweze kukidhi mahitaji yao ya msingi kama chakula, malazi na gharama za masomo.

Kwa kawaida vyuo vina utaratibu wa kumruhusu mwanafunzi aingie darasani na kupata huduma nyingine za kitaaluma kama mikataba, anakuwa amekamilisha kulipa gharama za masomo, hivyo Bodi hainabudi kuhakikisha kwamba inapeleka kwa wakati fedha za mikopo kwenye vyuo, kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaweza kusoma bila vikwazo.

Ikumbukwe pia kwamba hakuna mwanafunzi kati ya waombaji wa mikopo anaweza kusoma kama hajapata mahitaji ya msingi kama chakula na malazi.

Jambo la kutia moyo ni kwamba serikali ya awamu ya tano imeonyesha umakini kwa kupeleka fedha za mikopo vyuoni kwa wakati, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma, hali iliyokuwa ikisababisha usumbufu na malalamiko kutoka kwa wanafunzi.

Angalau sasa tunashuhudia uwazi na uwapo wa taarifa za kutosha kwa umma kuhusiana na mchakato mzima wa kutoa mikopo kuanzia wanufaika wa kundi la kwanza hadi la mwisho.

Kadhalika, kumekuwapo na utaratibu mzuri wa kukata rufani kwa wale ambao hawakupewa fedha au kupewa kiasi kidogo. Jambo la kufurahisha ni kuwa Bodi imekuwa ikizishughulikia rufani hizo kwa wakati na kutoa mrejesho.

Kwa mfano, tulishuhudia migomo na vurugu za wanafunzi, ambazo lengo lake likuwa ni kuvishinikiza vyuo na Bodi kuwapa fedha zao.

Tunaamini kuwa wakati huu ambao vyuo vinafunguliwa, vyuo na menejimenti za vyuo watakuwa wameshawasiliana kuhusiana na taratibu za kupelekwa kwa fedha hizo na kuwapatia wanafunzi.

Ikumbukwe kuwa vyuo vikuu vilifungwa kwa zaidi ya takribani miezi miwili kuanzia Machi hadi Juni kutokana na tishio la ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona, hivyo upo umuhimu mkubwa wa kuhakikisha wanafunzi wanaanza kusoma mapema, ili kukamilisha programu zao za masomo.

Tunatarajia kuona wanafunzi kwa upande wao wanakuwa watulivu kwa kufuata taratibu na maelekezo yanayotolewa na Bodi pamoja na uongozi wa vyuo, ili kuondoa usumbufu usio wa lazima.

Vilevile, wanafunzi tunaendelea kuwakumbusha na kuwasisitiza wafahamu kuwa fedha hizo wanapewa kwa kuwa wazazi na walezi wao hawana uwezo, hivyo wazithamini na kuzitumia vizuri ili wapate elimu ya juu kwa ajili ya kuwakomboa kimaisha.


Kwamba; serikali ingezitumia kwa ajili ya kuwahudumia wananchi kwa huduma za msingi za jamii pamoja na kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, hivyo wakumbuke kwamba wanawajibika kuzirejesha baada ya kuhitimu na kupata kipato ili na wenzao wakope.

Tunatarajia kusikia bodi ikitoa taarifa kuhusiana na utaratibu mzima wa kuwapatia mikopo wanafunzi. Kwa kawaida mikopo hutolewa kwa awamu kwa makundi ya wanufaika.

Hata hivyo, hatutarajii kuona inachukua muda mrefu kukamilisha utoaji kwa wanafunzi wote wanaostahili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Matendo haya yakomeshwe mitihani inavyoendelea sasa

**MWAKA** huu, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) ilinasa walimu watano kwa tuhuma za wizi na udanganyifu wa mitihani ya darasa la saba, katika mikoa ya Tabora na Manyara.

Wakuu wa TAKUKURU wa mikoa hiyo, Mussa Chaulo (Tabora) na Holle Makungu, wanatoa taarifa za matukio hayo kwa vyombo vya habari Oktoba mwaka huu na kuwataja watuhumiwa kwa majina.

Udanganyifu na wizi wakati wa mitihani ni visa vinavyoibuka na kupotea ingawa kuna jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali kwa ajili ya kukabiliana na vitendo hivyo.

Miongoni mwa jitihada hizo ni kuwapo kwa Kamati za Mitihani za Mikoa na Wilaya zinazosimamia sheria, kanuni na taratibu, lakini bado wapo wajanja wachache wanaoendelea kufanya 'usanii'.

Hivyo ni muhimu wahusika kushiriki katika vita ya udanganyifu na wizi wa mitihani, kwa kuwa vitendo hivyo vina athari kubwa kwa mtu mmoja mmoja kuanzia mwanafunzi, mwalimu, shule na taifa.

Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) linawatuhumu baadhi ya walimu wakuu na wasimamizi wasio waaminifu kushiriki katika vitendo vya udanganyifu wakati mitihani inapokuwa inaendelea na kusababisha wanafunzi kufutiwa matokeo.

Mbinu mojawapo ambazo zinadaiwa kutumiwa ni wakuu wa shule kula njama na wasimamizi wa mtihani na kukubaliana kuchukua baadhi ya mitihani ikishafunguliwa na kuipeleka nje ya chumba cha mitihani, ili kupata majibu yanayotolewa kwa watahiniwa waliokusudiwa.

Ni vyema kuwaacha wanafunzi wafaulu kwa akili zao wenyewe kwa sababu kama hawawezi itakuwa vigumu kusonga mbele na katika mazingira hayo itakuwaje wakipelekwa shule za vipaji, watakuwa na uwezo darasani?

Nikumbushe kwamba, mitihani ya taifa ya upimaji kwa wanafunzi wa kidato cha pili, ilianza jana ukihusisha shule za sekondari 4,948 za Tanzania Bara, na inataendelea hadi hadi Novemba 20 mwaka huu.

Hiyo ni ratiba iliyotolewa juzi jijini Dar es Salaam, na Katibu Mtendaji wa NECTA Dk. Charles Msonde, wakati akizungumza na vyombo vya habari.

Kwa mujibu wa Dk. Msonde, Novemba ya kila mwaka ni mwezi wa upimaji na mitihani mbalimbali ya kitaifa na kwamba baada ya kidato cha pili kumaliza watafuata wanafunzi wa kidato cha nne.

Dk. Msonde anasema, wanafunzi wa kidato cha nne wataanza mitihani Novemba 23 hadi Desemba 11 mwaka huu, wakati wale wa darasa la nne watafanya mitihani yao Novemba 25 na 26.

Wakati huu wa mitihani, ni muhimu usifanyiwe udanganyifu ama wizi ili wanafunzi wafaulu kwa akili zao wenyewe badala ya kulazimisha wavuke huku wakiwa hawana uwezo darasani.

Wenye mtindo huo wakumbuke kuwa wizi na udanganyifu wa mitihani ni vitendo vinavyoweza kuporomosha elimu nchini, kwa kuwa watapatikana wasomi ama wataalamu wasio na sifa.

Hivyo ni muhimu hatua ziendelee kuchukuliwa dhidi ya wote wanaobainika kukiuka sheria, taratibu na miongozo inayotolewa na kusababisha kuwapo kwa udanganyifu wa wizi wa mitihani nchini.

Lakini ni vyema zaidi walimu wakuu wanasimamie kanuni na weledi kwenye masuala ya mitihani ili kuunga mkono juhudu za serikali za kutaka kutoa elimu bora kwa jamii na kuinua viwango vya ufaulu kwa wanafunzi.

Vitendo vyovyote vya udanganyifu na wizi wa mitihani, visiwe sehemu ya ustaarabu wa Watanzania, bali vipingwe na kila mdau wa elimu, ili visiendelee kuwapo na kuathiri sekta ya elimu.

Wahusika watambue kuwa vitendo hivyo pia vinalivunjia taifa heshima, hivyo wanaotuhumiwa kujihusisha na masuala hayo waache watimize wajibu wao inavyotakiwa wa kusaidia watahiniwa kufanya siyo kuwafanyia mitihani.

Matarajio ya Muungwana ni kuona mitihani ya kidato cha pili inayoendelea sasa, ikifuatiwa na ya kidato cha nne na ya darasa la nne, ikifanyika bila kuingiliwa na wizi ama udanganyifu.

# Asasi yawezesha kituo cha yatima

**Na Christina Mwakangale**

KITUO cha kulelea watoto yatima cha Amani kilichopo Kata ya Nsalala jijini Mbeya, kimepokea msaada wa vifaa vya shule pamoja na sabuni za kufulia kutoka Sauti ya Mama Africa Foundation (SAMAFO), ikiwa ni mwendeleza wa asasi hiyo kusaidia makundi maalum yenye mahitaji.

Akikabidhi msada huo, Mchungaji wa Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini Magharibi Ushirika wa Mabatini, Mbeya, Michael Simkoko, alisema jamii inapaswa kuwahudumia watoto hao baada ya kuondokewa na wazazi.

"Jamii inapaswa kutowatesa yatima na kuwanyanyasa, wala kuwanyang'anya mali zao baada ya wazazi wao kufariki.

Kupitia kitabu cha kutoka 22: 24, kinasema 'Usimtese mjane yeyote aliyefiwa na mumewe, wala mtoto yatima. Ukiwatesa watu hawa katika neno lolote, nao wakanililia mimi, hakika yangu nitasikia kilio chao na hasira yangu itawaka moto," alisema Mchungaji Simkoko.

Mkurugenzi Mtendaji wa asasi hiyo, Tabitha Bugali, alisema huo ni mwendeleo wa kutoa msaada kwa makundi kama hayo.

Alisema kituo hicho kilikabidhiwa kalamu za kuandikia, madaftari, sabuni za kufulia pamoja na mafuta ya kupaka.

Akizungumza kwa niaba ya kituo cha Amani, baada ya kupokea vifaa hivyo, Mchungaji Bahati Mshani aliishukuru SAMAFO, kwa upendo na kwamba si mara ya kwanza kupokea msaada kutoka asasi hiyo.

"Ni zaidi ya mara mbili kufika kituoni hapa, nathamini mchango huu na kuomba wana Mbeya na Tanzania kwa ujumla, kutambua suala la watoto yatima ni jukumu letu sote.

Tunaomba jamii kusaidia ili kuwakomboa watoto hawa, kielimu na kisaikolojia," alisema Mchungaji Mshani.

Akizungumza kwa niaba ya watoto wenzao baada ya kupokea vifaa hivyo, Elizabeth George, alisema wanajiona kuwa na wazazi wao wapo hai na kuwapa hamasa ya kusoma.

Alisema baada ya kuhitimu masomo na kufanikiwa watasaidia watoto yatima kielimu.



Mkurugenzi wa Tigo, Simon Karikari (katikati), akishiriki tamasha la rangi ambalo huadhimishwa kila mwaka na jamii wa watu wenye asili ya India, lililofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na kudhaminiwa na kampuni ya simu ya Tigo Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wito kutafuta matibabu ya watoto wenye usonji

**Na Richard Makore,** MWANZA

JAMII imeshauriwa kutafuta matibabu kwa watoto wenye matatizo ya usonji badala ya kufikiria imani za kushirikiana.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini Mwanza na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Serikali la Li-Tafo (Living Together Austin Foundation), Shangwe Mhaya, alipozungumza na Nipashe.

Alisema tatizo hilo linawakuta watoto ambapo wanashinda kuchangamana na watu, kuwasiliana na watu na kuzoea mazingira mapya.

Aliongeza kuwa tatizo hilo linawakuta watoto wengi na kwamba wameandaa hafla maalum, ili kutafuta fedha na vifaa mbambali kuwasaidia.

Alisema tatizo hilo linasababishwa na kuharibu kwa mfumo wa fahamu, hivyo mtoto kukabiliwa na shida ya kupata usingizi, kuchangamana na watu, kusahau vitu pamoja na kutozoea mazingira mapya.

Kwa upande wake, Dk. Nuru Ndomondo, Mkurugenzi Msaidizi wa shirika hilo, alisema haijajulikana chanzo cha tatizo hilo.

Dk. Ndomondo alisema mtoto anayezaliwa akiwa na shida hiyo anashindwa kupata usingizi, kuchangamana na watu wengine na kwamba tiba yake wanatibu tabia.

Alisema Novemba 15, mwaka huu, wameandaa harambee maalum ambayo itaongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, kwa ajili ya kutafuta fedha na vitu mbalimbali ili kusaidia familia 40 zenye watoto wa namna hiyo.

Aidha, alisema wanatarajia pia kuandaa harambee nyingine ili kutafuta Sh. milioni 500 kwa ajili ya kujenga kituo cha kusaidia watoto wenye shida hizo.

Aliwaomba wadau kujitokeza katika harambee hiyo, ili kuokoa maisha ya watoto hao.

# Wahitimu afya kuhitimu CUHAS

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

WAHITIMU 620 wa Chuo Kikuu cha Katoliki cha Afya na Sayansi Shirikishi (CUHAS) Bugando jijini Mwanza, wanatarajia kuhitimu taaluma mbalimbali za afya mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu wiki ya mahafali ya 13 itakayofanyika Jumamosi wiki, Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Paschalis Rugarabamu, alisema wahitimu wa chuo hicho wamefanya vizuri kikazi.

"Licha ya mahafali hayo, lakini chuo chetu cha CUHAS kinatarajia kuwa na udahili wa jumla ya wanafunzi 3,289 watakaoendelea na masomo katika taaaluma mbalimbali kwa mwaka wa masomo 2020/2021," alisema.

Prof. Rugarabamu alisema wanafunzi watakaohitimu chuoni hapo ni 51 wenye taaluma ngazi ya diploma ya mionzi, maabara 89, famasia 74 pamoja na watano kuhitimu shahada ya ualimu wa uuguzi.

Alisema wengine watakaohitimu shahada ya uuguzi ni 67, maabara ya afya wanane, ufamasia 83, udaktari 212, ikiwa 15 shahada ya uzamili ya afya ya jamii, wawili uuguzi wa watoto, shahada za uzamili mbalimbali za utabibu 13 na mmoja shahada ya uzamivu.

Aidha, alibainisha kuwa chuo hicho kinatoa mafunzo mbalimbali katika vitivo na kutoa taaluma katia fani za udaktari, uuguzi, ukufunzi wa wauguzi, ufamasia, maabara za afya, mionzi, uzamili katika elimu za afya ya jamii pamoja na uzamili katika microbiologia ya vinasaba.

Vilevile, uzamili wa fani mbalimbali za kitabibu (Masters of Medicine) uzamili katika uuguzi wa watoto, uzamivu (PhD) pamoja na elimu ya maabara, mionzi na famasia katika ngazi ya stashahada.

# Mvua yaua wawili, yajeruhi watatu

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WATU wawili wamepoteza maisha katika Manispaa ya Kigoma Ujiji na wengine watatu kujeruhiwa na kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kigoma Maweni kufuatia mvua iliyonyesha Novemba 8, mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, ACP James Manyama, akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kufafanua kuwa mvua iliyonyesha majira ya saa tano asubuhi ikiambatana na radi ilisababisha kijana, Yassin Khalfan mwenye umri wa miaka 18, kupoteza maisha baada ya kupigwa na radi wakati akicheza na wenzake.

Manyama alieleza kwamba mtu mwingine ambaye anakadiriwa kuwa na umri wa miaka 10 alipoteza maisha kwa kusombwa na maji ya mvua hiyo na mwili wake kukutwa kandokando ya mto katika eneo la Kibirizi.

"Natoa tahadhari huu ni mwanzo wa mvua, watu wachukue tahadhari ili kuepusha maafa zaidi," alionya kamanda huyo.

Baraka Simon, shuhuda wa tukio la aliyepoteza maisha kwa kupigwa na radi, alisema siku ya tukio wakati wa mvua wakiwa ndani walikuwa wanapiga kelele kabla ya mwenzao kupigwa na radi.

"Walikuwa wanapiga kelele, mimi nikawambia nyamazeni kisha nikawasha simu na kuzima ndipo nilipoona amepigwa radi na kuanguka chini," alisema.




Ofisa msimamizi wa mawakala wa Benki ya Azania, Emmanuel Ndege (kulia), akimkabidhi cheti cha ushiriki mmoja wa mawakala wa benki hiyo, Evarist Lyakurwa kutoka Masonga Business Centre baada ya mafunzo ya siku moja yaliyofanyika Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Lema, Nyalandu waingia matatani

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

SIKU chache baada ya aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, kukamatwa kaunti ya Kajiado nchini Kenya, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu, amekamatwa pia.

Nyalandu ambaye amewahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Mbunge wa zamani wa Jimbo la Singida Mashariki, katika serikali ya awamu ya nne, alikamatwa akitaka kwenda nchini Kenya.

Akizungumza na NIPASHE, Mkuu wa Wilaya ya Longido mkoani Arusha, Frank Mwaisumbe, alithibitisha kushikiliwa kwa viongozi hao wa CHADEMA.

Alisema Nyalandu alifuatiliwa na kukamatwa akiwa na gari ambalo siyo lake na ambalo halijasajiliwa, hakuwa na hati ya kusafiria, bila simu yoyote ya mkononi na kwamba alitaka kuvuka mpaka kuelekea upande wa Kenya.

"Tulivyomhoji alisema anaishia Namanga, lakini tuligundua kuwa nia yake ilikuwa kutaka kuvuka mpaka, baada ya kumkamata yeye na gari tukamrudisha nchini," alisema Mwaisumbe.

Alisema walimwachia huru kwa masharti ya kuleta nyaraka za gari jana na hati ya kusafiria na kama akishindwa kufanya hivyo atachukuliwa sheria.

Vile vile, Mwaisumbe alisema Nyalandu atafikishwa mahakamani kwa kosa la kutembea na kuendesha gari lisilo na nyaraka zozote na halijasajiliwa.

Wakati huo huo, DC huyo alithibitisha kukamatwa kwa Lema ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CHADEMA Taifa, aliyekamatwa katika kaunti ya Kajiado nchini Kenya, baada ya kuvuka mpaka kwa kutumia pikipiki kupitia njia za panya.

"Familia ya Lema ilikuwa na nyaraka na vibali vyote muhimu vya kusafiria na kuvuka mpaka kwenda nchi jirani pamoja na hati za kusafiria, isipokuwa Lema ambaye hakuwa na vibali vyovyote. Tukamuacha bila kumchukulia hatua yoyote na ndipo akakodisha pikipiki na kupita njia za panya," alisema na kuendelea:

"Tuliwasiliana na wenzetu wa Kenya Kajiado, askari wakamkamata, kwa sababu baada ya kushuka kwenye pikipiki aliingia kwenye gari, walikuwa wameandaa gari huko huko kwenye njia ya vumbi, upande wa Kenya, wakamkamata. Kwa kweli walitoa ushirikiano askari hao maana walimpeleka kwenye kituo cha polisi."

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya alisema: "Yaani wanataka kufanya kama ukimbizi wa kisiasa, sio kwamba hati za kusafiria hawana, ukipita kwa hati ya kusafiria unaulizwa kama unataka kuuawa serikali hiyo hiyo ikupe hati ya kusafiria, ikugongee muhuri upite, wewe unaonekana kabisa unapita pale, sasa unataka kuuawa vipi."

"Kuna concern wana raise (kuna jambo wanataka ionekana) ili waonyeshe kwamba wanakimbia kuna tatizo, kumbe hakuna wanajifanyisha," alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

**DADA YAKE LEMA**

Dada wa Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini (ambaye hakutaka kutajwa jina lake gazetini), alisema jana alikuwa amepumzika kuna mtu akampigia simu kwamba mbona kaka yake anashikiliwa Kajiado? Akamjibu kuwa labda ni maneno ya kizushi mitandao ya kijamii.

"Nikashtuka nikamwambia kata simu, nikajaribu namba za kaka yangu na mkewe zikawa hazipatikani, huyo mtu akanitumia 'link' inayoonyesha kuwa Lema anakamatwa Kajiado, nikawasha gari nikaenda kwake, kwa kuwa tunaishi kila mmoja kwenye nyumba yake, kufika nyumbani kwake nikakuta kijana wa kazi na msichana wa kazi nikawauliza Lema ameenda wapi? Wakajibu amesafiri, nikawauliza tena wameondokaje? Wakasema ameondoka asubuhi (jana)na watoto na mke wake, basi nikarudi nyumbani kwangu," alisema dada wa Lema.

Alisema akiwa njiani alikutana na mdogo wake aliyekuwa anaishi na Lema (amekataa kumtaja jina lake gazetini) akamuuliza kuhusu kusafiri kwa kaka yao akasema amesikia amekamatwa nchini Kenya na hajui lolote, lakini aliondoka akasema anasafiri kwenda Kenya.

"Basi ndio ilivyoishia naona kama hakutaka kumuaga mtu yoyote kwenye familia kwa kuwa kutaleta maumivu, hatujui chochote kinachoendelea, mimi sijui chochote na tangu uchaguzi umemalizika sikuonana naye," alisema.

MARCAS DEBT COLLECTORS AND AUCTIONEERS (T) LTD.

MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONERS LTD,

MNADA WA HADHARA

**MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONERS LTD,** kwa idhini tuliyopewa na **Hughes Agricuture (T) Ltd,** P.O.Box 75344 Dar es Salaam tutauza matrekta (4) kwa njia ya mnada; mnada huo utafanyika katika ofisi za **Hughes Agriculture, maeneo ya Tazara karibu na Daraja Mfugale,** siku ya **14th Novemba 2020.** Wanunuzi wote mnakaribishwa kukagua matrekta tarehe **13th Novemba 2020** kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 9 alasiri.



**MASHARTI YA MNADA**
1. Mshindi atalipa 25% papo hapo baada ya nyundo ya dalali kushuka na kiasi kinachobakia yaani asilimia 75% italipwa ndani ya siku (14) baada ya siku yam nada, mnunuzi atakaeshindwa kulipa asilimia 75% zilizobakia atapoteza ushindi wake na hatarudishiwa kiasi cha awali cha 25% na mali hii itanadishwa tena.
2. Bidhaa zitauzwa kama zilivyo.
3. Wanunuzi watatakiwa kufika na vitambulisho vyenye picha zao ambavyo vinatambulika na serikali.
4. Mnunuzi atalipa gharama za kodi na uhamisho.
5. Sio lazima mnunuzi mwenye bei ya juu kuwa mshindi, dalali ana haki ya kumchagua mnunuzi atakae kidhi vigezo

Kwa maelezo Zaidi wasiliana kwa simu; 0752 722222/ 0713 268383

# Makandarasi wa majengo wafundwa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MAKANDARASI wa ujenzi wa majengo wametakiwa kufanya kazi zao kwa kuzingatia taaluma na weledi mkubwa, ili kujenga majengo imara na kwa muda mwafaka ili kukidhi mahitaji ya soko.

Wito huo ulitolewa na Meneja wa Wakala wa Majengo (TBA) Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Elias Tilya, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuelezea kazi ambazo zimefanyika kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mhandisi Tilya alisema katika jukumu la kusimamia kazi za ujenzi au ukarabati wa majengo ya serikali na taasisi zake, wamekuwa wakikutana na changamoto ya makandarasi ambao sio waaminifu, hali ambayo imekuwa ikichelewesha ukamilishaji wa miradi.

"Utakuta mkandarasi unamlipa fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi ya ujenzi wa mradi X, yeye anachukua fedha ile na kuipeleka kwenye mradi wake mwingine ... jambo hilo limekuwa likichelewesha kukamilisha kwa mradi husika," alisema na kuongeza:

"Pia wakati mwingine hupelekea ama kusitisha mkataba na kumpa mkandarasi mwingine au kutoa onyo kwa mkandarasi husika."

Tilya alisema kuwa kwa sasa jengo la ghorofa la nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Nyasa limekamilika na linatumika. Pia jengo la ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Madaba limekamilika na kwa sasa linatumika.

Alieleza kuwa ujenzi wa jengo la utawala la Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa ambalo mkandarasi ni SUMA JKT na TBA ni wasimamizi wa mradi huo ambao unaendelea vizuri na hatua za ujenzi.

Alisema kuwa mradi mwingine ambao TBA inausimamia ni ukarabati wa maabara ya maji katika bonde la Mto Nyasa, ambapo kwa muda mrefu ukarabati huo ulisimama kutokana na sababu za kiufundi katika mkataba ila kwa sasa unaendelea, mkandarasi ni Kampuni ya Intercity ya jijini Dar es Salaam.

Alieleza kuwa changamoto nyingine ambayo tunakabiliana nayo ni maduka mengi kutokuwa na vifaa vya ujenzi ambavyo vinatakiwa kwenye mkataba husika, hali ambayo inatulazimu kuviagiza kutoka nje ya Ruvuma na kusababisha miradi hiyo ujenzi wake kudorora.

**Utakuta mkandarasi unamlipa fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi ya ujenzi wa mradi X, yeye anachukua fedha ile na kuipeleka kwenye mradi wake mwingine ... jambo hilo limekuwa likichelewesha kukamilisha kwa mradi husika**




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akiongea na wafanyabiashara wakubwa katika wilaya hiyo, kwenye hafla iliyokuwa imeandaliwa na benki ya NMB ya kukaa pamoja na kubadilishana mawazo katika lengo la kuboresha huduma kwa manufaa ya pande zote mbili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Moto wa ajabu wazua taharuki Kahama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kitongoji cha Lugela Mlimani, Halmashauri ya Mji wa Kahama, mkoani Shinyanga, wamekumbwa na taharuki baada ya kuzuka kwa moto wa ajabu ambao chanzo chake hakijajulikana unaoungunza samani za ndani pekee.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wakazi wa kitongoji hicho kwa nyakati tofauti, walisema moto huo umeunguza magodoro na vitanda, katika nyumba tisa za eneo hilo.

Japhet Kaliwa, Mwenyekiti wa Mtaa wa Shunu, alisema moto huo ulianza kuunguza vitu mbalimbali Oktoba 4, mwaka huu, katika nyumba zaidi ya tisa na kwamba wakazi wa kitongoji hicho wanashindwa kwenda kwenye shughuli za uzalishaji mali kwa kuhofia usalama wa mali zao kuteketea kwa moto huo wa ajabu.

"Kumeibuka kwa moto ambao umekuwa ukiwaka ndani na kuunguza samani za ndani pekee, hasa umekuwa ukitokea wakati tumeelekea kwenye shughuli zetu, tatizo hili limewaathiri wakazi wangu kwa sasa wanaogopa kulalia magodoro kwa hofu ya kulipuka kwa moto huo ambao umekuwa ukijiwasha wenyewe," alidai Kaliwa.

Naye Upendo Bundala, alisema kuwa familia yake imeathiriwa na moto huo kutokana na kuungua kwa samani mbalimbali yakiwamo magodoro yote na kulazimika kulalia mifuko ya sandarusi.

Alidai kuwa, amepata hasara ya zaidi ya Sh. 500,000 baada ya mali zake kuteketea kwa moto huo ambao chanzo chake hakijajulikana na kuiomba serikali kwa kushirikiana na wenyeviti wa mitaa na kata kulitafutia ufumbuzi wa haraka ili moto huo usiendelee kuteteza mali za ndani.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya Kahama, Anamringi Macha, aliwatoa hofu wakazi wa kitongoji hicho kuwa tayari kuna kamati imeundwa ya kuchunguza chanzo cha moto huo ambao hauunguzi nyumba, lakini mali za ndani pekee na kuwataka kuendelea kuchukua tahadhari zaidi.

"Acheni kutuhumiana kwa tukio hili, vyombo vyetu vya usalama vipo kazini ili kubaini chanzo cha uwapo wa moto huo wa ajabu, endeleeni na shughuli za uzalishaji mali huku mkichukua tahadhari na moto huu," aliongeza Macha.

Naye Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alithibitisha kutokea kwa moto huo na Joseph Dida, mmoja wa waathirika ameunguliwa na vitu vya ndani vyenye thamani ya Shilingi milioni mbili.

Kamanda alisema uchunguzi wa awali unaonyesha matukio yote ya kuunguliwa kwa vitu vya ndani bila kuungua kwa nyumba hutokea wakati wa mchana wamiliki wake wakiwa kwenye shughuli za ujenzi wa taifa na nyumba hizo hazina umeme.

# Polisi Mara yaonya watakaofanya vurugu

**Na Ambrose Wantaigwa,** MUSOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mara limeonya kwamba litachukua hatua kali dhidi ya mtu au kikundi chochote kitakachofanya maandamano.

Jeshi hilo limesema kwamba hali ya usalama imeimarishwa baada ya kukamilika uchaguzi mkuu na kuwataka wananchi kuendelea na shughuli zao kama kawaida.

Onyo hilo limetolewa na Kamanda wa Polisi mkoani humo, Daniel Shilla, ambaye alisema jeshi hilo limejipanga kulinda maisha na mali za raia wakati wote na kuonya kwamba watamchukulia hatua kali mtu au kikundi chochote kitakachohamasisha uvunjifu wa amani kwa kutumia siasa.

Alisema wanasiasa kama wananchi wengine wanayo haki kutafuta suluhu na ufumbuzi wa matatizo yao kwenye vyombo vya kisheria ikiwamo mahakama badala ya kuhamasisha matumizi ya nguvu yakiwamo maandamano.

"Wakati Jeshi la Polisi linatekeleza majukumu ya kulinda maisha na mali za raia, tutachukua hatua kali kwa mtu au kikundi chochote katika jamii kinachohamasisha uvunjifu wa sheria na matumizi ya nguvu bila upendeleo wala uonevu," alisema Shilla.

Alisema chombo pekee chenye uwezo kisheria kutoa maamuzi na tafsiri ya kisheria nchini ni mahakama pekee, na kwamba kila mwananchi ana haki ya kusikilizwa na sio matumizi ya nguvu na vurugu.

Aliwataka wananchi wote mkoani humo kushirikiana na jeshi hilo, kwa kutoa taarifa kuhusu njama zozote za kuhujumu amani katika maeneo yao baada ya kukamilika uchaguzi mkuu, ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

# Wakulima wafunguka kupaa bei ya korosho

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKULIMA wa korosho Mkoa wa Lindi, wameanza kujenga matumaini mapya ya maisha, kufuatia kuimarika kwa bei ya zao hilo.

Matumaini hayo yanatokana na kupanda kwa bei ya zao hilo kutoka Sh. 2,388 kwa kilo kwa minada iliyopita hadi Sh. 2,407 kwa mnada uliofanyika Jumamosi.

Hata hivyo, wakati bei ya korosho ikipanda kwa mwendo wa kusuasua, idadi ya kampuni zilizojitokeza kununua korosho inazidi kushuka kutoka 10 hadi tano.

Wakizungumza na Nipashe kwenye mnada wa nne uliofanyika Mtaa wa Tulieni, Manispaa ya Lindi, baadhi ya wakulima Shani Juma, Habibu Mohamedi, Sharifa Yusufu na Daniel John waliohudhuria, walieleza kuwa na uhakika kuimarika kwa maisha yao licha ya bei kupanda kwa kiwango kidogo.

"Walisema licha bei ya korosho kuonekana kusuasua, lakini wameanza kuwa na matumaini kidogo kuboreka kwa maisha yao.

Aidha, wameeleza kwamba kazi ya kuhudumia mikorosho ni ngumu, hivyo licha ya kuongezeka kwa bei ya manunuzi kwa kila mnada unapofika, upo umuhimu kwa wanunuzi wakafikiria upya kuongeza viwango vya bei, ili wakulima wawe na nguvu katika kuzalisha zaidi zao hilo.

Walisema bei ya mauzo ya korosho kwa misimu iliyopita 2016/2017, ilikuwa na unafuu zaidi, kwani bei ilipanda kutoka Sh. 3,500 kufikia Sh. 4,000 kwa kila kilo moja ikilinganishwa na bei ya hivi sasa ya Sh. 2,388 na Sh. 2,407.

Ofisa Ushirika Mkoa wa Lindi, Edmundi Massawe, akitangaza viwango vilivyofikiwa na kampuni katika mnada huo wa nne, alisema bei ya juu ni Sh. 2,407, huku Makamu Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao, Mohamedi Masoud, aliwahoji wakulima kama wapo tayari kuuza, na kujibu ndio.

Akizungumza wakati wa mnada huo, Masoud aliwasisitiza wakulima kuhakikisha wanaziandaa korosho zao kwenye ubora unaokubalika, ili kuongeza mnyororo wa thamani na heshima kwenye soko la mauzo kuanzia ngazi husika ya vijiji, kata, wilaya, mkoa hadi taifa.

Masoud alisema msimu wa mwaka huu korosho sio nyingi kwenye vyama vya msingi, hivyo upo umuhimu mkubwa wa kupokea zao hilo likiwa katika mazingira ya usafi unaochangia mkulima kupata bei nzuri.

Katika mnada huo wa nne tangu msimu wa mauzo wa mwaka huu uanze, zaidi ya tani 57 za korosho zimepata wanunuzi kupitia kampuni tano zilizojitokeza siku hiyo.



Askari polisi wilayani Kahama akisikiliza maelezo kutoka kwa wanakikundi wa Mwime 2 na Iserenge Gold Mine ambao wanagombea eneo la uchimbaji dhahabu wilayani humo, mkoani Shinyanga mwishoni mwa wiki. **PICHA: MOHAB DOMINICK.**

# TAKUKURU yaokoa mil. 107/-

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Ruvuma katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba imefanikiwa kuokoa fedha zaidi ya Sh.107,478,845 kutokana na uchunguzi mbalimbali ambao umefanyika.

Akizungumza hivi karibuni na waandishi wa habari, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma, Hamza Mwenda, alisema katika kutimiza moja ya majukumu yake, taasisi hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali walifanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha.

Mwenda alieleza kuwa Sh. 488,000 zimepatikana kutokana na marejesho ya madeni ya Benki ya Wananchi Mbinga (MCB), fedha ambazo ziliwekwa kwenye akaunti ya Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo iliyoko Benki Kuu.

Alieleza kuwa Sh. 94,420,845 zimeokolewa kutokana na uchunguzi unaoendelea katika vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) wilayani Songea na Sh. 1,436,000 ni marejesho ya madeni ya Muungano SACCOS ya wilayani Namtumbo.

Alisema Sh. 2,465,000 ni marejesho ya madeni ya Mbinga Teachers SACCOS na Sh. 1,779,000 ni marejesho ya madeni ya Mbinga Kurugenzi SACCOS ambapo fedha zote za SACCOS ziliwekwa kwenye akaunti za vyama husika.

Alifafanua kuwa shilingi 5,890,000 ni fedha iliyookolewa wilayani Nyasa kwenye deni feki alilowekewa Ufunuo Chirwa na mtu wa Taasisi ya Maboto kwani mkopaji alistahili kulipa Sh. 4,000,000 lakini aliwekewa deni la jumla ya 9,890,000 kwa njia za ujanja ujanja.

Aidha, mkuu huyo alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano na TAKUKURU katika mapambano ya kupinga rushwa kwa kukemea, kuzuia vitendo vyote vyenye viashiria ya rushwa katika jamii na kwenye ofisi za umma.

## Wakaguzi maeneo ya malisho wapewa somo

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI mkoani Morogoro imewaagiza wakaguzi wa maeneo ya malisho na rasilimali za vyakula na mifugo kufanya kazi zao kwa kusimamia sheria, kanuni na taratibu ili kulinda afya ya walaji na mifugo.

Aidha, imewagiza kutoa elimu ya kutosha kwa wadau waliopo kwenye mnyororo wa thamani kwenye tasnia ya vyakula vya mifugo na kufanya hivyo kutatua changamoto ya matumizi ya vyakula na rasilimali za vyakula vya mifugo visivyo na ubora.

Agizo hilo lilitolewa na Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, kwenye hotuba yake kwenye ufunguzi wa mafunzo kwa wakaguzi na wataalamu wa mifugo yaliyofanyika mjini Morogoro.

Mhandisi Kalobelo, aliwataka wakaguzi na wataalamu wa mifugo kufanyia kazi elimu na ujuzi wanaoupata katika mafunzo mbalimbali kwenye vikao kazi, ili kuwasaidia wafugaji kufuga kisasa na kuboresha uchumi wao.

Aliwataka wakaguzi hao na wataalamu wa mifugo baada ya kumaliza mafunzo kuandika ripoti ya mafunzo hayo na kuonyesha namna watakavyotoa elimu hiyo kwa wafugaji katika kuwezesha wazalishaji na wafugaji wa vyakula vya mifugo kuendelea kufuga kisasa zaidi.

"Yapo mazoea kwa watumishi walio wengi wanaoshiriki mafunzo kutoonyesha elimu au ujuzi wanaopata kwenye mafunzo kwenye vikao kazi, hivyo hakutakuwa na tofauti kati ya mtumishi aliyepata mafunzo na ambaye hakupata na badala yake anaendelea na utaratibu wake wa kila siku, " alisema Mhandisi Kalobelo.

Aliwahimiza kuwa mafunzo hayo yawe chachu kwao na kuwasaidia wafugaji kuzalisha mifugo kwa tija kwa kutumia vyakula kutoka maeneo yaliyosajiliwa na kutambulika kisheria ili kuongeza mchango wa sekta ya mifugo katika kuinua uchumi ngazi ya kaya.

Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Malisho na Vyakula vya Mifugo, Dk. Asimwe Rwiguza, alisema mafunzo hayo yalitolewa kwa wakaguzi na wataalamu hao, ili kuwezesha kutatua changamoto za ubora na viwango hafifu vya vyakula vya mifugo vinavyotumiwa na wafugaji wengi.

Alisema kuwa kumeonyesha zipo athari za ukuaji hafifu kwenye kuku, mbwa, nguruwe na sungura.

Alisema mafunzo hayo yalishirikisha wakaguzi wa chakula cha mifugo kutoka kanda ya mashariki inayoshirikisha mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Pwani na Dodoma.

Nipashe
TESA
Jumanne Novemba 10, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

**TMA inavyojipanga kuufikia umma athari za tsunami**



Ukurasa 12



Ukurasa 14

**Moto kuteketeza shule, inawezekana miaka ya uchaguzi ikawa ya balaa**



Ukurasa 13

Watoto hawatakamatika...

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# 'Laiti jamii ingeijua hali ya watu wenye ualbino isingewanyanyapaa'

MAUA mwenye watoto wanne amewapa watoto wake majina yanayoakisi hali halisi na machungu aliyotembelea licha ya kwamba jamii haiwezi kufahamu kilichofichwa ndani ya majina hayo yenye asili ya Kipare.

Mmoja wa mabinti zake anaitwa Leda na mwanaume amempa jina la Nasu yote hayo yanaeleza ujumbe wa kukataliwa na chuki dhidi ya watoto wake ulioko ndani ya familia ya mumewe. Leda ni kifupisho cha Ledaiwe ikitafsirika 'asiyependeka' wakati Nasu inaamaanisha 'nasua' yaani 'aliyekataliwa' na baba au jamaa za ukoo wake.

Maua ni mfano wa kinamama wanaoakisi majina yenye matendo ya kuwakataa watoto na kuwatelekeza mama zao, huku wakilaumiwa kwa kuzaa watoto wenye hali zisizokubalika na jamii wakiwamo wenye ualbino (People With Albinism), mgongo wazi, ulemavu wa viungo na usonji (autism).

Ndiyo maana jamii ya watu wenye ualbino, wanaitaja mienendo ya kuwakataa watoto kuwa imekuwa chanzo cha PWA kukataliwa na baba na familia yake na kusababisha wengi kukosa msaada wa wazazi na kulelewa zaidi na mama zao.

Aidha, mama hao kulaumiwa kwa kuzaa mtoto mwenye hali ya ualbino.

Kutokana na kuwasusa watoto na kuwatelekeza mama zao wamelazimika kulelewa na mzazi mmoja hasa mama, anasema Seif Kondo.

Kondo Ofisa Uraghibishi wa Taasisi ya Under the Same Sun (UTSS), inayotetea na kulinda haki na ustawi wa PWA nchini, anasema yote hayo ni kutokana na jamii kukosekana uelewa kuhusu hali ya ualbino na anafafanua zaidi.



Irene Kishe akionyesha kikuza maandishi 'dome lens' kinachotumiwa na wenye ualbino ili kuongeza uoni. Kulia ni Seif Kondo, wakiwa kwenye mkutano uliozungumzia hali ya watu wenye ualbino. **PICHA: MWANDISHI WETU**

### HALI YA WENYE UALBINO

Anasema hali ya wenye ualbino ni ukosefu au upungufu wa rangi ya asili 'melanin' kwenye macho, ngozi na nywele, kwa mujibu wa UTSS.

Anasema zipo aina kuu mbili za ualbino wa macho ambao kitaalamu huitwa OA (ocular albinism) ambao husababisha macho kukosa rangi ya asili, lakini si kila mwenye tatizo hilo anaweza kuwa ni mwenye ualbino.

Aina nyingine hali ya ualbino ni ukosefu wa rangi ya asili kwenye macho, ngozi na nywele kitaalamu huitwa Oculocutaneous albinism (OCA) na hiyo imeeenea zaidi duniani na kwa Afrika Mashariki kuna idadi kubwa zaidi ya PWA wenye ukosefu wa rangi ya asili ya ngozi, macho na nywele.

Anakosoa mazoea ya kuwatelekeza na kuwakataa pamoja na kuwakejeli kinamama wanaozaa watoto wenye ualbino kwa sababu hilo si suala la mzazi mmoja bali ni wote wamechangia kuzaliwa kwa PWA.

"Ualbino hauambukizi. Unarithiwa kutoka kwa wazazi wawili. Ni baba na mama lazima wawe na nasaba za ualbino hivyo mmoja hawezi kufanikisha kuzaliwa mtoto mwenye ualbino. Haiwezekani." Anasema Kondo.

Anaongeza: "Ni jeni (gens) za baba na mama wote wawili ndizo zinazohusika. Ni lazima wawe na nasaba za ualbino ndipo anapopatikana mtoto. Ni sharti wote wawili wawe na nasaba za hali ya ualbino baba kwenye mbegu za uzazi na mama kwenye mayai ya uzazi."

Kondo anasema kwa Afrika Mashariki watu 19 mmoja ana vinasaba vya hali ya ualbino na kwamba inawezekana baba na mama wakawa na hali ya ualbino lakini wakapata watoto wasio na ualbino.

Anaeleza kuwa ni kutokana na mbegu za baba au mayai ya mama kuwa na tabia za jeni tawaliwa (recessive genes) ambazo inatokea zikazidiwa nguvu na jeni tawala (dominant genes) ambazo hazina hali ya ualbino.

"Licha ya kwamba katika hatua hizo wazazi hawatazaa mtoto mwenye ualibino lakini anakuwa `keria' kwamba ana nasaba za hali ya ualibino." Anaongeza Kondo.

Anakumbusha kuwa jamii haifahamu kuwa ni wazazi wote wawili wanaohusika na kupatikana mtoto mwenye ualbino hivyo hakuna sababu ya kumfukuza mama na mtoto wake na kumkejeli kuwa amekuzalia PWA.

Anaeleza kuwa hali ya ualbino ni ya viumbe wote kuanzia binadamu, wanyama, mimea na wadudu na kwamba si ugonjwa bali ni hali ya kimaumbile ya kurithiwa na isiyoambukiza.

### CHANGAMOTO KIELIMU

Kondo anasema kwenye kusoma darasani na kuona vitu mbalimbali PWA wanakabiliwa na uoni hafifu kwa sababu uwezo wa macho kwenye kuona ni asilimia 25 na kwa mataifa mengine PWA wanachukuliwa kuwa ni wasioona kwa mujibu wa sheria.

Tatizo la kutooana linatokana na kukosa rangi ya asili kwenye macho kunakosababisha mwanga kuumiza macho hasa nyakati za mchana lakini kwa wanafunzi darasani wanashindwa kusoma ubaoni na pale herufi zinapokuwa ndogo inakuwa ni tatizo zaidi.

"Wanashindwa kusoma na kutimiza ndoto zao kitaaluma kwa vile inawawia vigumu kusoma shuleni, wengine huacha shule, walimu wanawadhibu wakidhani ni wajeuri."

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA FAUSTINE FELICIANE

# TMA inavyojipanga kuufikia umma athari za tsunami



Mawimbi ya tsunami yakitishia usalama wa maisha na mali katika moja ya miji ya Afrika : **PICHA MTANDAO**

HIVI karibuni Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) pamoja na mamlaka nyingine duniani zimeadhimisha Siku ya Tsunami Duniani, inayofanyika Novemba 5, kila mwaka, safari hii kauli mbio ikiwa ni 'utayari kwa wimbi la tsunami'.

Kwa Tanzania TMA inaitumia siku hiyo kutoa elimu juu ya athari zitokanazo na tsunami na kuelezea kwa kina nini maana ya tetemeko hilo na namna linavyotokea.

Mtaalamu wa utabiri wa hali ya hewa wa TMA, Joyce Makwata, akizungumzia tsunami anasema: "Watu wanaweza wakajiuliza nini maana ya tsunami? Kwanza ni maneno mawili yaliounganishwa 'tsu' likiwa na maana ya bandari na 'nami' lenye maana ya wimbi, kwa ujumla tsunami ni mfululizo wa mawimbi makubwa ya maji yanayofika urefu wa mita 30 na kusafiri kwa kasi ya kufika kilomita 950 kwa saa. Mawimbi haya yanaweza kutokea kutokana na tetemeko la ardhi chini ya bahari, milipuko ya volkano au ya nyuklia, haya yote yanaweza kusababisha mawimbi makubwa ya kufika ukubwa huo niliosema ambayo sasa tunaita tsunami," anasema Joyce.

> Septemba, 2018 Tanzania ilishiriki katika zoezi la kukabiliana na janga la tsunami katika Bahari ya Hindi.

Aidha, Mkurugenzi wa Huduma za utabiri wa mamlaka hiyo, Dk Hamza Kabelwa, anasema pia tsunami inaweza kutokea kwa kuanguka kwa vimondo baharini ambavyo husababisha kuhamisha kwa ghafla kiasi kikubwa cha maji bahari ambayo yana nguvu kubwa na kusafiri kwa kasi.

**MATUKIO YA TSUNAMI**

Dokta Kabelwa anasema matukio ya tsunami kwa kawaida huripotiwa mara chache, hata hivyo hutokea ghafla na madhara yake ni makubwa kuliko aina nyingine za majanga.

"Mfano wa tukio la tsunami ni lile la mwaka 2011 lililotokea nchini Japan lilitokana na tetemeko la ardhi chini ya bahari ambalo lilikuwa na ukubwa wa kipimo cha ritcha 9.0 katika pwani ya bahari ya Pasifiki," anasema Dk. Kabelwe.

Aidha, anataja jingine kuwa ni la mwaka 2004 lililotokea Indonesia na mawimbi yake kufika kwenye Pwani ya Afrika Mashariki Tanzania ikiwamo.

Anasema kutokana na matukio hayo na athari zake, serikali za nchi za ukanda wa Bahari ya Hindi kupitia kamisheni yake ya masuala ya bahari (Intergovernmental Oceanographic Commission- IOC) inayosimamiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Utamaduni (UNESCO) zimefanya kazi kubwa ya kujenga mfumo wa tahadhari ya tsunami unaohusisha upimaji na utoaji wa tahadhari.

"Kwa upande wa Tanzania, TMA inashirikiana kikamilifu na idara ya uratibu wa maafa ya ofisi ya Waziri Mkuu katika kuhakikisha tahadhari ya tsunami inatolewa ipasavyo na hatua stahiki zinachukuliwa ili kupunguza maafa," anasema Dk. Kabelwa.

**ELIMU KWA JAMII**

Dokta Kabelwa anasema tsunami inaleta athari kubwa ndani ya dakika chache baada ya kutokea na husababisha vifo vya maelfu ya watu ndani ya muda mfupi na uharibifu mkubwa wa miundombinu kutokana na mafuriko yake.

Programu mbalimbali za elimu za kujenga uelewa kwa jamii zimekuwa zikiendeshwa katika maeneo hatarishi ya tsunami.

"Katika kuhakikisha mfumo wa tahadhari unafanya kazi ipasavyo, kila mwaka Tanzania hujihusisha katika maandalizi ya kukabiliana na tsunami kwa kujihusisha na mazoezi ya kupima uwezo wa miundombinu ya mawasiliano katika nchi za ukanda wa bahari ya Hindi," anasema Dk. Kabelwa.

Aidha, anasema TMA itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia majukwaa mbalimbali juu ya athari za tsunami.

Anaeleza kuwa programu mbalimbali za elimu za kujenga uwelewa kwa jamii zimekuwa zikiendeshwa katika maeneo hatarishi ya tsunami.

Maeneo hayo ni yale ambayo yanazunguka bahari ambapo kwa ukanda wa Afrika Mashariki ni Tanzaia na Kenya nchi ambazo zinapakana na Bahari ya Hindi.

"Katika kuhakikisha mfumo wa tahadhari unafanya kazi ipasavyo, kila mwaka Tanzania ujihusisha katika maandalizi ya kukabiliana na tsunami kwa kushiriki katika mazoezi ya kupima uwezo wa miundombinu ya mawasiliano katika nchi za ukanda wa bahari ya Hindi," Dk. Kabelwa anaongeza.

Anasema Septemba, 2018 Tanzania ilishiriki katika zoezi la kukabiliana na janga la tsunami katika Bahari ya Hindi.

"Zoezi lile lilishirikisha wadau wa nchi 24 zinazozunguka Bahari ya Hindi, na hufanyika kila baada ya miaka miwili, kwa mwaka huu lilifanyika Oktoba 20 na kuhusisha wadau na taasisi na mamlaka za mkoa wa Dar es Salaam," anasema mtaalamu huyo.

Aidha, amesema katika mwaka huu jukwaa la uratibu wa maafa la Mkoa wa Dar es Salaam (DarMAERT) lilitumika katika kupima utayari wa mifumo ya mawasiliano na miongozo ya kiutendaji katika kukabiliana na tsunami kwa Wilaya za Ilala na Kinondoni.

Aidha, Dk. Kabwelwa anasema TMA itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia majukwaa mbalimbali juu ya athari za tsunami, huku ikitegemea zaidi vyombo vya habari kutoa kufikisha taarifa zao kwa wananchi.

"Vyombo vya habari ni mdau muhimu zaidi katika kufikisha elimu na taarifa mbalimbali za hali ya hewa, vyombo vya habari ni daraja imara na la umuhimu kati ya mamlaka na wananchi," anaongeza Kabelwa.

# 'Laiti jamii ingeijua hali ya watu wenye ualbino isingewanyanyapaa'

**INATOKA UK.11**

**UFUMBUZI**

Akizungumzia ufumbuzi Ofisa wa Uhusiano na Uraghibishi wa UTSS Irene Kishe, anasema cha msingi na cha lazima ni kutoa elimu ili watu wafahamu hali ya ualbino na chanzo chake. Aidha, akizungumzia kusoma anasema ni vyema kuwaweka PWA viti vya mbele darasani, kuandika herufi kubwa ubaoni zinazosomeka, lakini walimu na wahadhiri wanaweza kuwasaidia kwa kuwapa matini au notes zinazosomeka. Pamoja na hilo kufikisha shuleni vitabu vyenye maandishi makubwa kwa ajili ya PWA.

Irene anasema ni vyema wakati wa kufundisha walimu na wahadhiri wakatamka na kuandika mathalani, zinapoandikwa mbili na mbili ni nne pia zitamkwe..."

Anataja vikuza maandishi kama 'monocular' na lensi ya kukuza maandiko ya 'dome lens' vinatumiwa kuwasaidia wanafunzi wanaoishi na ualbino walioko shuleni na vyuoni.

Hata hivyo, anasema ni lazima PWA wafunguke na kueleza kuwa hawaoni herufi badala ya kukaa kimya darasani au vyuoni, akitoa mfano wake kuwa zamani alipokuwa chuo kikuu, alikuwa hawezi kusoma ubaoni na kushindwa kuandika wakati mhadhiri anafundisha na kuandika ubaoni.

Anasema alipoulizwa kwanini haandiki alimjibu kuwa haoni herufi ubaoni na huo ukawa mwanzo wa mwalimu kuwapa wanafunzi matini (notes) na kwamba si yeye pekee bali wengine zaidi ambao hawana ualbino walikuwa na tatizo la kushindwa kusoma.

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Watoto hawatakamatika...

## • Saikolojia inatumiwa kuwaundia fikra, mtazamo mpya na kujiamini



Mkufunzi Geoffrey Leons, akiwaelekeza jambo wanafunzi ikiwa ni sehemu ya mafunzo yanayotolewa kwenye programu ya 'setting myself for success'. **PICHA: PEAK PERFORMANCE**

WATOTO wenye umri kati ya miaka nane hadi 18 wana kila sababu ya kufurahia ushindi na mafanikio baada ya kuanzishwa programu maalumu ya mafunzo kuwasaidia kujitambua, kuwa na mtizamo chanya na jinsi ya kutumia uwezo ulio ndani yao kufikia malengo na kupata mafanikio makubwa kimaisha.

Programu hiyo ya mafunzo inakuja baada ya kugundua kuwa malezi katika ngazi ya familia, shuleni na jamii hayalengi kuwajenga watoto kisaikolojia yaani kujitambua, kujiamini na kuwa wabunifu na pia mambo haya hayafundishwi shuleni.

Kampuni ya Peak Performance International ndiyo inayoanzisha programu hiyo, kwa mujibu wa Meneja Mkuu Upendo Kimbe, mafunzo yanayotolewa yanalenga zaidi kumjenga mtoto kisaikolojia ambayo ni asilimia 80 ya mafanikio yake.

Anaiambia Nipashe hivi karibuni jijini Dar es Salaam kuwa wanasayansi mbalimbali duniani walifanya utafiti wakagundua kwamba mafanikio yanachangiwa na asilimia 20 tu za ujuzi na zilizobakia 80 zinatokana na saikolojia ya mtu ambayo ni imani, tabia, utamaduni na mtazamo wa kifikra.

"Mafanikio ya mtu yanatokana na saikolojia yake ndiyo maana hata ambao hawajakwenda shule wameweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa sana ukilinganisha na wale walioenda shule, lakini wana mtazamo hasi."

"Kwa mfano mtu ambaye hajasoma labda ameishia darasa la saba lakini anaamini anaweza kuwa mfanyabiashara mkubwa ina maana imani yake itaiambia jambo linawezekana na ninaweza kuwa mfanyabiashara nijitahidi na nifanikiwe," anasema Kimbe.

Kimbe anakumbusha kuwa ili mtu aweze kufanikiwa katika biashara au masomo yake anatakiwa awe na mtazamo wa kifkra na imani yake na mtazamo wake uwe chanya kwamba nitafanikiwa.

"Ukiwa na mtazamo chanya kila hatua unayochukua hata kama ni ndogo itakuelekeza katika mafanikio," anasisitiza Meneja Mkuu.

Anakumbusha kuwa baada ya kugundua hilo Peak Performance, inaamua kuanzisha mafunzo mbalimbali ya kuwafanya watu wajitambue, wajue uwezo walionao ndani yao na jinsi ya kutumia huo uwezo walionao kufikia malengo na kupata mafanikio katika maisha yao.

"Mpaka sasa tuna programu za vijana kuanzia miaka nane hadi 15 na kuanzia miaka 15 hadi 18, wanachuo ambao wapo chuoni, lakini ambao wanakaribia kuingia kwenye ajira na wale ambao tayari wapo kwenye kazi," anasema.

Akielezea vijana anasema: "Wakati wa mafunzo tunafundisha watoto kujitambua, kuwa na mtizamo chanya, yaani wawe na imani kwamba kila kitu kinawezekana, wanaweza kila kile ambacho wanataka kufanikisha katika maisha yao licha ya kwamba kuna vikwazo ndani yao wanatakiwa kujiambia mimi mtoto nina uwezo mkubwa sana ambao nimeumbwa nao na kuifanya ndoto yangu ije kutokea."

Anaongeza kuwa mbali na hilo, watoto wanafundishwa hasara za kuwa na mienendo na tabia hasi kwenye mafanikio na jinsi ya kuzibadili ili zije kuwa na mafanikio.

"Tunawafundisha hatua za kubadilisha tabia na jinsi ya kuzifanya tabia hizo zisirudie tena ili waweze kutimiza malengo yao binafsi," anasema Kimbe.

Tangu waanze kutoa mafunzo Tanzania na nchi nyingize za Afrika Mashariki, elimu imeleta mabadiliko makubwa kwa watoto wengi na kwamba wameona kuna mengi ya kujivunia.

"Tumeona maisha yao yamebadilika, wameweza kufikia malengo yao waliojiwekea kwa mfano kulikuwa na mwanafunzi wa Kenya, kila mara alikuwa anakuwa mtoto wa mwisho darasani na walimu wake walishamwambia kuwa wewe si kitu na hautaweza kufanikiwa katika maisha.

Meneja Mkuu wa Peak Performance anasema anaporudi shuleni mtoto huyo anaonyesha mabadiliko na alianza kufanya masomo yake vizuri, akaanza kuwa wa kwanza darasani na sasa hivi amemaliza sekondari anasomea kozi za udaktari.

Anasema wazazi wengi mara nyingi wanaangalia zaidi matokeo kama mtoto anafeli au anafaulu zaidi darasani na kama akifeli wanamwadhibu au wanatafuta mwalimu mwingine ambaye atamfundisha masomo hayo hayo bila kujua kufeli kwake kunaweza kuwa kumesababishwa na saikolojia yake iliyo hasi ambayo inawezekana amejengewa shuleni au nyumbani kwa wazazi wake kusema kuwa huwezi hili au hautaweza lile.

Kinginge ni kumwambia mtoto acha kila anapojaribu kudadisi kitu na hapo ndipo unapozuia kipaji cha mtoto wako kuwa mbunifu ansema Kimbe. Anaeleza kuwa wazazi wakilitambua hili kwamba baadhi ya matatizo ya watoto wao ni ya kisaikolojia zaidi wanaweza kupata njia bora ya kuyatatua na kuchangia katika mafanikio yao ya baadaye.

"Na njia ya kutatua matatizo hayo ni kuwaleta watoto kwenye programu zetu za watoto ambazo wakati wa mafunzo tunafundisha watoto kujitambua na kuwa na mtazamo chanya.

Anasema kwa mfano, mtoto anakuja na tabia ya uvivu, anaelimishwa kuwa uvivu unaweza kuwa na madhara gani katika kufikia mafanikio yake na mbali na hilo, pia wanatoa huduma hizo katika shule mbalimbali hapa nchini kwa faida ya wanafunzi, lakini kwa faida ya shule kwa sababu mwanafunzi akibadilika tabia na mtazamo ufaulu wa shule pia unaongezeka.

Anasema kwa mfano kila mwaka kampuni ya Peak Performance inaandaa mafunzo ya watoto katika shule mbalimbali, lakini wana programu nyingine za wazi ambapo kila mzazi anaweza kumleta mtoto wake akapata mafunzo.

Mara nyingi majukwaa hayo yanafanyika wakati shule zikiwa zimefungwa na wanaandaa sehemu maalumu ya kuwafundisha watoto kujitambua, kuwa na mtazamo chanya na kubadilika tabia zinazowakwamisha kimaendeleo.

> Na njia ya kutatua matatizo hayo ni kuwaleta watoto kwenye programu zetu za watoto ambazo wakati wa mafunzo tunafundisha watoto kujitambua na kuwa na mtazamo chanya.

Akielezea zaidi programu hizo mkufunzi Geoffrey Leons, anasema Peak Performance Tanzania, ilianzisha mafunzo hayo tangu mwaka 2005 kwa lengo la kuwajenga vijana na wanafunzi shuleni kwenye tabia, imani na kuwaelekeza kuwa na mtazamo chanya.

Anasema baadhi ya programu ambazo ni pamoja na 'setting myself for success' inahusisha wanafunzi wa darasa la kwanza mpaka la nne kwa lengo la kuwajengea uwezo binafsi na kuwafanya wajue wajibu wao shuleni.

Programu nyingine ni 'youth leadership academy' ni mafunzo maalumu kwa ajili ya kuwaandaa vijana na kuwafanya kuwa viongozi katika maisha yao ili wafahamu jinsi gani wanaweza kufikia ndoto zao inatolewa kwa wanafunzi wenye miaka 13 hadi 18.

"Pia tunafundisha 'candidates program' kwa watahiniwa, imejikita zaidi katika kuwasaidia na kuwajengea fikra chanya pamoja na kuwafanya wajue wanahitaji nini kwenye maisha yao hasa katika mitihani yao." Anasema Leons.

Mbali na hilo pia wanafunzi wanafundishwa 'youth the camp' ambazo ni mbinu za kuwajenga vijana namna gani ya kutimiza malengo yao, kuwajenga nidhamu katika masomo na namna ya kupanga malengo na kufanikiwa ili wawe na kesho bora, anaongeza.

Walionufaika ni pamoja na wanafunzi wa Canossa, Baobab, The Indian School Arusha na Shaaban Robert nyingine ni shule za msingi za Dar es Salaam Independent School, Aga Khan, Sunrise, Prime na St. Constantine's International School zote za Arusha.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Moto kuteketeza shule, inawezekana miaka ya uchaguzi ikawa ya balaa



Shule ya Mivumoni ni miongoni mwa zilizoungua hivi karibuni ni matukio yaliyoripotiwa na kusababisha taharuki miongoni mwa wazazi na wanafunzi. **PICHA: MTANDAO**

MIEZI mitatu iliyotangulia kufanyika kwa uchaguzi mkuu Oktoba 28, ilikuwa na matukio kadhaa ya moto kuteketeza shule, ambayo watafiti walioangalia kilichotokea miaka iliyopita na mikasa ya moto ya hivi karibuni wanapata picha kuwa inaendana kwa mazingira yake . Walichohoji ni kwanini nyakati za uchaguzi, yaani mwaka unaofikia uchaguzi mkuu au miezi inayotangulia kura kupigwa, ndiyo shuleni zinapozidi kuchomwa moto? Ni mazingira ambayo yanaashiria kuwa dhamira halisi inahusika katika kuizusha ambako suala la migongano ya kisiasa halipo, hivyo inabakia kuhisi imani potofu.

Siyo kwamba moto unaanzishwa kwa njia za ajabu ila dhamira ya kuzusha moto huo inaelekea kuendana na tuhuma za jadi kuwa nyakati za uchaguzi mkuu huwa zinafuatana na vielelezo kadhaa vya kuvunja haki za binadamu, hasa kuhusiana na kuuawa kwa watu wenye ualbino. Hatari hiyo ilipungua ilianza kupotea uchaguzi mkuu wa 2010 baada ya kampeni kubwa za ndani na mashirika tetezi ya kimataifa, serikali na vyombo vya dola zikalazimika kuchukua hatua na hali hiyo ikaondoa kadhia ya mauaji ya vikongwe kwa tuhuma za ushirikina. Uchaguzi ukawa si tishio.

Ambacho hakikugunduliwa na kisingeweza kugunduliwa ni kuwa wakati mauaji ya watu wenye ualbino na vikongwe yanakomeshwa, washirikiana na wateja wao kutoka dunia ya siasa (na kwa upande fulani biashara) walishahamia kwingine. Dalili zinaonyesha kuwa moto ulianza kitambo kwa mfano Shauritanga mwaka 1994, lakini ilipamba moto katika muongo uliofuata, kuanzia mwaka 2000 wa uchaguzi mkuu hadi 2009 kuelekea uchaguzi mkuu mwingine. Mwaka huu kumekuwa na moto miezi ya Julai, Septemba na Oktoba ambayo ilitikisa mikoa kadhaa na kote huko ni shule zinaunguzwa.

Kama maduka na hata viwanda havihusiani na moto moja kwa moja ambako mwekezaji atavihitaji iweje shuleni? Ni swali ambalo linaendelea kufanyiwa tafakari.



Wako waliofanya utafiti ni kiasi gani shule zimejiandaa kukabiliana na moto kama inazuka maeneo hayo, na ulipozuka katika shule ya bweni wilayani Kyerwa mkoani Kagera, mmiliki wa shule alitupwa ndani na mabweni yote yakafungwa. Punde Rais John Magufuli, akaamuru atolewe kifungoni na hakuna hakika kama bado yapo mashtaka anayokabiliana nayo, kwani siyo rahisi kusimamia uwepo wa kinga za kutosha dhidi ya moto, kuanzia miundombinu ya umeme hadi vifaa vya kuzima moto, tena viwepo kila bweni. Shule za binafsi na hata za serikali hazina uwezo wa kujipanga kikamilifu kwa hilo.

Jiji la Dar es Salaam lilishangaza zaidi kwa kuwa na matukio matatu ya moto katika shule tatu ndani ya miezi miwili, kwani Julai 5, bweni la Shule ya Kiislamu Ilala liliungua moto na kuua watoto watatu. Julai 17 siku 123 baadaye, moto ukaunguza Shule ya Sekondari Kinondoni na hapo Agosti 31, ikaungua Shule ya Sekondari Mivunoni. Ni mazingira ambayo yanaleta shaka kitakwimu ni udhaifu wa miundombinu hadi kusababisha moto? Kwanini ajali zitokee wakati mmoja?

Wimbi hilo ni kama lilikamilika siku 14 baadaye mkoani Kagera, ambako Shule ya Msingi ya Byamungu wilayani Kyerwa, nayo pia iliungua moto na watoto 10 wakapoteza maisha yao. Kana kwamba haitoshi, Septemba 27 Shule ya Sekondari Istiqama mjini Tabora iliungua moto, ila hakuna upotevu wa maisha ulioripotiwa, ni uharibifu mkubwa wa mali za shule na binafsi uliooonekana. Siku iliyofuata, Septemba 28, bweni la Shule ya Sekondari ya Yustus huko Mwanza liliungua tena asubuhi ya saa 2:00 kwa kile kilichodaiwa ni hitilafu ya umeme. Hapakuwa na upotevu wa maisha ila mali za wanafunzi 22 wa bweni hilo ziliharibiwa kabisa, hali iliyoendana kiasi fulani na matukio ya awali.

Utafiti uliyofanyika kimsingi umeelekeza jitihada katika kujua viwango vya kujiandaa kwa majanga ya moto, ambako jibu lilikuwa wazi kuwa kiwango ni kidogo, kwani shule hazina vifaa vya kitaalamu vya kuzima moto, na hata vingekuwapo, wanafunzi katika bweni wasingeweza kuvitumia. Kuwa na uwezo huo kimsingi inahitaji uwekezaji wa kina katika miundombinu, na ajira za ziada katika utawala na usimamizi wa rasilimali au usalama wa wanafunzi, uwekezaji ambao uko nje ya uwezo wa wajasiriamali katika sekta ya elimu. Wakilazimishwa kufikia viwango hivyo karo zitakazohitajiwa wazazi hawatamudu.

Wapo waliotaja ongezeko la wanafunzi katika mabweni kuwa ni chanzo kimojawapo cha mazingira hatarishi, lakini ukiangalia unakuta bweni liliungia lenye wanafunzi 22 waliopoteza vifaa vyao katika masanduku. Idadi hiyo ya wanafunzi siyo mrundikano kwa hali yoyote ile, hasa ikikumbukwa kuwa kuna wakati wanafunzi hadi sita walikuwa wanatumia chumba kimoja cha kulala Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, badala ya wanafunzi wanne, au hata wawili kwa baadhi ya mabweni. Kusema kuwa idadi ya wanafunzi watakaotumia bweni iangaliwe wakati shule inaandikishwa ni sawa, ila isiongezewe chumvi.

Wako maofisa wa kikosi cha kuzima moto waliohojiwa na watafiti wakasema shule zinatakiwa kufikia viwango vya usalama kuhusiana na majanga ya moto. Licha ya kuwa hawakufafanua kwa upana zaidi wanahitaji maandalizi gani na kanuni zipi zitumike, itakumbukwa kuwa Waziri wa Fedha, Dk. Philip Mpango alifuta kodi ya ukaguzi wa tahadhari ya moto ambayo ilikuwa inatozwa majengo yote ya biashara na shughuli nyingine (kama siyo majengo ya serikali) kuwa ni moja ya masuala ya usumbufu ya ukaguzi yanayoweka vikwazo katika biashara, hasa kuanzisha biashara mpya.

Kama maduka na hata viwanda havihusiani na moto moja kwa moja ambako mwekezaji atavihitaji iweje shuleni? Ni swali ambalo linaendelea kufanyiwa tafakari.

# Ampongeza JPM kuamua kuapishwa Dodoma

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

ASKOFU Mkuu wa Huduma ya The World Ministries, Damas Thadey, amempongeza Rais Dk. John Magufuli, kwa kuandika historia kubwa kutokana na uamuzi wake wa kuamua sherehe za kuapishwa kwake kwa mara ya kwanza kufanyika jijini Dodoma.

Pongezi hizo alizitoa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema uamuzi wa Rais Magufuli kufanya sherehe za kupishwa makao makuu ya chama na serikali yametengeneza ukurasa mpya wa utawala wake kwa kuwa huko nyuma shughuli hizo zilikuwa zikifanyika jijini Dar es Salaam.

"Toka nchi hii ipate uhuru wake mwaka 1961, chini ya Baba wa Taifa hayati Mwalimu Nyerere, sherehe za kuapishwa zote zilikuwa zinafanywa mkoani Dar es Salaam, lakini kwa awamu hii ya Rais Magufuli ambaye amethubutu hata makao makuu ya serikali kuhamishia Dodoma, sina budi kumpongeza kutokana na tukio hili la kistoria," alisema.

Alimwomba rais atakayechukua kijiti cha Dk. Magufuli baada ya kumaliza muhula wake, kuheshimu hatua hiyo ya kufanyia sherehe ya kuapishwa Dodoma zikiwamo na zingine zote za kitaifa ili kuleta maana halisi ya uwapo wa makao makuu ya serikali.

Kwa upande wake Askofu wa Kanisa la International Evangelism Sinai Ipagala Dodoma, Selvester Thadey, aliwataka Watanzania kuwaombea wabunge ambao kwa mwaka huu kumekuwapo na sura mpya tofauti na miaka ya nyuma.

"Tunatakiwa kuwaombea wabunge ili watuwakilishe vizuri sisi wananchi kwa sababu wengi wao mwaka huu ni wageni kabisa katika muhimili huu," alisema.

# Watumishi wa umma watakiwa kuzingatia maadili ya utumishi

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WATUMISHI wa umma nchini wametakiwa kuendelea kuzingatia maadili ya utumishi ili kuondoa malalamiko kwa wananchi wanaopata huduma kwao.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, alitoa kauli hiyo wakati alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa wizara hiyo kwenye mafunzo yaliyofanyika mwisho wa wiki, jijini hapa.

Dk. Nzuki aliwataka watumishi hao kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuzingatia maadili ili kuondoa malalamiko kwa wananchi wanaofika kupata huduma kwao.

Alisema, wizara imeamua kutoa mafunzo hayo kwa wafanyakazi wake ili kuboresha utendaji wa wao kila idara za kiutumishi.

Alisema tatizo la wafanyakazi kuchanganya mafaili na madokezo ndiyo sababu iliyowasukuma kutoa mafunzo hayo ili kuboresha utendaji wa kazi.

Aidha, alisema mafunzo hayo yatawajengea uwezo zaidi wa kikazi ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi wakifika kwenye ofisi zao.

Mkurungenzi wa Idara ya Nyuki, Dk. Ezekiel Mwakalukwa, alishukuru wizara kwa kutoa fursa ya mafunzo kwa wafanyakazi.

Aliahidi baada ya mafunzo hayo wataenda kufanya kazi kwa bidii na kuondoa makosa ya kiutendaji yaliyokuwa yakifanyika kimakosa.

Aidha, Mkurungenzi wa Utawala na Rasilimali Wizara ya Maliasili na Utalii, Lusius Mwenda, alisema mafunzo hayo yameshirikisha wafanyakazi zaidi ya 150, kutoka idara zote za wizara.

Mwenda, alisema kwenye mafunzo hayo kutakuwa na mada mbalimbali zitakazo wasilishwa ili kuwajengea uwezo wa kikazi wafanyakazi hao.

Alizitaja baadhi ya mada hizo kuwa ni maadili ya utumishi zitakazowasilishwa na mtu kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) pamoja na utumishi wa umma.

Alisema mada nyingine ni namna ya kutunza mafaili kwenye masijala za wazi na siri na kuandika madokezo bila kujirudia pamoja na mada kuhusu upimaji wa afya, ili kuweka afya za wafanyakazi kwenye hali nzuri.

Kadhalika, alisema mwisho wa mafunzo hayo watachangia damu ili kuokoa maisha ya watu wengine wanaohitaji damu kwenye hospitali za hapa na wafanyakazi watapewa chanjo ya homa ya manjano.




Mbunge mteule Jimbo la Nkenge mkoani Kagera, Florent Kyombo (kulia), akijisajili bungeni jana, kushoto ni Ofisa wa Bunge, Patson Sohba. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Msalaba Mwekundu yahamasisha umuhimu kujiunga

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHAMA cha Msalaba Mwekundu nchini (Red Cross) kimeitaka jamii kuwa na mwamko wa kujiunga na chama hicho ili kuwa na uwezo wa kutoa huduma ya kwanza katika maeneo mbalimbali na kuokoa maisha ya watu yanapotokea majanga.

Mratibu wa huduma ya kwanza kitaifa, Kheri Issa, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu, mwitikio wa jamii kujiunga na chama hicho.

Issa, alisema pamoja na kuwa wananchi wanakielewa chama hiko, mwitikio wa kujiunga bado mdogo ikilinganishwa na idadi ya watu iliyopo.

Alisema, wataendelea kutoa elimu ya umuhimu wa kujiunga na chama hicho ambapo mwanachama anaweza kutoa huduma ya kwanza pale linapokutana na janga lolote katika mikusanyiko.

"Tunaomba jamii itambue umuhimu wa kujiunga na Chama cha Msalaba Mwekundu kwa sababu kina umuhimu katika jamii," alisisitiza Issa.

Alisema kuwa wameamua kuhimiza suala la kujiunga katika chama ili kutoa msukumo kwa jamii kujitokeza kushiriki katika shughuli za kusaidia majanga mbalimbali yanapotokea.

Alifafanua kuwa mpaka sasa chama hiko kimefika katika mikoa 21, lakini lengo lao ni kuifikia mikoa yote hapa nchini.

"Bado tuna kazi ya kuielimisha jamii kuhusu namna ya kukijua Chama cha Msalaba Mwekundu, nia yetu ni kuona jamii nzima inakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kukubali kujitolea kwa ajili ya wengine," alisema Issa.

Alisema, kwa Mkoa wa Dodoma, chama hicho kimeweka tawi lengo ikiwa ni kuboresha utoaji wa huduma ya kwanza ikiwemo kukabiliana na idadi ya ongezeko la watu kutokana na kuwa makao makuu ya nchi.

Mkufunzi wa huduma ya kwanza kitaifa, Hamis Mrisho, alisema changamoto walizobaini katika utekelezaji wa majukumu yao kuwa ni pamoja na jamii kuwa nyuma katika kusaidia majanga yanapojitokeza.

"Jamii yetu bado haina uelewa wa kutosha juu ya kusaidia wengine, wengi wanadhani yanapotokea majanga ni kazi pekee ya Chama cha Msalaba Mwekundu, nawasihii wanajamii kupenda kujitolea kuwasaidia wengine hasa ukizingatia sisi sote ni ndugu," alisema Mrisho.



# Wazee waomba kupatiwa kadi za bima

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

ZAIDI ya wazee 500 waishio katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya wameiomba serikali kupitia Wizara ya Afya kutoa bima nyingine za afya ambazo zitawasaidia kutibiwa kwenye vituo vikubwa vya kutolea huduma hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari wanawake wa Mkoa wa Mbeya, waliowatembelea wazee hao, kwa lengo la kutoa msaada na kufahamu matatizo yanayowakabili, Makamu Mwenyekiti wa Tumaini la Wazee jijini humo, Gwantwa Mwakitalima, alisema miongoni mwa vikwazo vinavyoikabili kundi hilo ni kukosa bima ya afya ambayo itatumika pia kwenye hospitali.

Alisema kwa sasa bima walizopatiwa wazee hao zinatumika kwenye vituo vya afya na zahanati na kutokana na hali zao wangepaswa kupata matibabu kwenye hospitali.

"Hitaji letu kubwa kwa sasa ni wazee hawa wasiojiweza kupatiwa bima za afya ambazo zitawasaidia kutibiwa kwenye vituo vikubwa vya afya kwa sababu wanahitaji huduma bora za matibabu pamoja na vipimo kuliko ilivyo sasa wengi wao hutibiwa kwenye Kituo cha Afya cha Kiwanja Mpaka," alisema Mwakitalima.

Pia Mwakitalima aliiomba serikali na wadau wengine kuendelea kuwapatia mahitaji ya chakula, malezi na fedha kwa ajili ya matibabu wazee hao ambao wanatoka katika Kata ya Nonde, Itiji, Maendeleo na Majengo, kutokana na hali zao za kutokuwa na uwezo wa kutafuta pesa kwa ajili ya kujikimu.

Mtoa huduma ngazi ya jamii kutoka kikundi hicho, Rose Wilson, alisema moja ya vikwazo anavyokutana navyo katika kulihudumia kundi hilo ni wengi wao kutokuwa na uwezo wa kutembea kufika kwenye vituo vya kutolea huduma.

Kutokana na kikwazo hicho hulazimika kuingia gharama za kutafuta usafiri ili kuwafikisha kwenye maeneo ya kupata huduma katika kila Jumanne ya wiki.

Alisema wazee wengi wanakabiliwa na matatizo ya kupooza, presha na kisukari na kuwafanya wapoteze nguvu ya kujihudumia na kujitafutia riziki.

Miongoni mwa wazee waliofikiwa na kikundi cha wanahabari wanawake, Mariana Chande, alisema kutokana na uzee na magonjwa yanayomsibu yamemsababishia kushindwa kufanya shughuli yoyote ambayo inamkosesha kupata mlo wa kila siku.

Alisema wakati mwingine hukosa hela ya kula na hana msaada wowote zaidi ya kuitegemea jamii kumsaidia.

"Hapa nilipo sina msaada wowote kutoka kwa ndugu maana karibu wote walifariki naitegemea jamii ndio initunze kwa kunipatia chakula, hela za matibabu na malazi maana nikipata hivyo naweza kujikongoja kupika," alisema Chande.

John Mbindi, aliwaomba wadau wengine kuendelea kuwasaidia fedha za matibabu ikiwamo na yeye ambaye hadi sasa hawezi kutembea kwa sababu ya baadhi ya viungo vyake ambavyo ni miguu na mikono yake kupooza.

Katibu wa kikundi cha wanahabari wanawake mkoani humo cha Women of Purpose, Prakseda Mbulu, alisema licha ya kutoa baadhi ya mahitaji kwa wazee hao, lakini wanajukumu la kupaza sauti za kundi hilo ili waweze kusaidiwa.

Alisema wazee hao wanakabiliwa na matatizo lukuki, hivyo wanahitaji msaada wa hali na mali ili waweze kuishi kwa furaha.



Mmoja wa wanakikundi cha waandishi wa habari wanawake mkoani Mbeya Women of Purpose, Rukia Chasanika (katikati) , akitoa msaada wa baadhi ya mahitaji kwa Mariana Chande (aliyekaa ), jana. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Tumaini la Wazee jijini humo, Gwantwa Mwakitalima. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanaong'oa miti mipaka ya maji waonywa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

JUMUIYA za watumiaji maji wilayani Mbeya wameiomba serikali kuchukua hatua dhidi ya watu wanaong'oa miti inayopandwa kwa lengo la kuonyesha mipaka ya vyanzo vya maji, ili wasionekane wamevamia vyanzo hivyo wanapofanya shughuli zao.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Jumuiya ya watumiaji maji wa bonde dogo la Mto Mbalizi, Aron Dawson, wakati wa hafla ya kukabidhiwa pikipiki kwa ajili ya kuwarahisishia usafiri wa kwenda kulinda vyanzo vya maji.

Alisema baadhi ya watu wanaofanya kazi zao kuzunguka vyanzo vya maji wamekuwa na tabia ya kung'oa miti inayopandwa kama alama ya mpaka wa vyanzo vya maji na kisha kumega maeneo yanayokaribia vyanzo vya maji kwa ajili ya kuendelea na shughuli zao za kiuchumi.

"Tunaiomba serikali itusaidie kuwachukulia hatua watu hao kwa vile wanatusababishia hasara ya kununua miti mingine na pia wanahatarisha usalama wa vyanzo vya maji ambayo tunayatumia kama jamii nzima inayoyategemea," alisema Dawson.

Alisema kuwa uamuzi wa kupanda miti kama alama ya mipaka kuzunguka vyanzo vya maji ni utekelezaji wa sheria ya utunzaji wa mazingira ambayo inaelekeza wananchi kutofanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 kutoka mahali kilipo chanzo cha maji.

Akijibu kero hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Ofisa Tarafa ya Usongwe, Sadat Mtwale, alisema kuwa tabia hiyo haikubaliki na kuonya kuwa wale wanaong'oa miti hiyo wakibainika serikali itawashughulikia kwa mujibu wa sheria.

"Hatuwezi kuvumilia kuona watu wachache wakiendelea kuhatarisha maisha ya jamii nzima kwa kuharibu vyanzo vya maji ambavyo ndio vinatusaidia wote kupata maji, tukiwabaini hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema Mtwale.

Hata hivyo, Mtwale aliwaagiza wenyeviti wa vijiji na vitongoji vilivyo jirani na vyanzo vya maji kuwa walinzi namba moja kwa kulinda vyanzo hivyo vya maji na kutoa taarifa ama kuwachukulia hatua watu wote watakaobainika wanaingilia maeneo ya vyanzo vya maji na kufanya shughuli za kiuchumi.

Akizungumzia makabidhiano ya pikipiki hiyo, Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Bonde la Ziwa Rukwa, Watson Mwalingo, alisema Wizara ya Maji imeamua kuwawezesha wananchi kulinda vyanzo vya maji kwa kuwapatia vifaa mbalimbali kwa ajili ya kazi hiyo.

Alisema vifaa hivyo vya kusaidia jumuiya za watumiaji maji kulinda vyanzo vya maji ikiwamo pikipiki kwa ajili ya kurahisisha usafiri vimetolewa na serikali kupitia kurugenzi ya maji.

## Rungwe yakabiliwa urejeshaji hafifu mikopo

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, inakabiliwa na urejeshaji hafifu wa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu hali inayosababisha vikundi vingine kushindwa kunufaika.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Omary Mungi, alisema hayo wakati wa akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya urejeshaji mikopo kwa vikundi mbalimbali vya ujasiriamali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Alisema kati ya Sh. milioni 332 ambazo halmashauri hiyo ilikuwa imekopesha mpaka mwezi Machi mwaka huu ni Sh. milioni 82.4 pekee ndizo zimesharejeshwa na vikundi hivyo ambayo ni sawa na asilimia 25 nusu ya lengo.

Alisema kwa mujibu wa utaratibu wa mikopo hiyo, ilitakiwa mpaka sasa asilimia 50 iwe imerejeshwa kwa ajili ya kukopesha vikundi vingine, lakini kutokana na tatizo hilo la urejeshaji hata fedha walizokopesha katika robo ya mwisho ni kidogo.

"Asilimia 75 ya fedha ambazo tulivikopesha vikundi ukiacha hizi za leo (juzi) bado hazijarejeshwa, sasa mikopo hii inatolewa bila riba ya aina yoyote, lakini bado wananchi wanakuwa wazito kurejesha, hii inatakiwa irejeshwe ili tukopeshe vikundi vingine," alisema Mungi.

Aliwataka wananchi wanaokopeshwa fedha hizo kuwa waaminifu ili wawe na sifa za kukopesheka wakati mwingine na kwamba wanatakiwa wazitumie kwa malengo yaliyokusudiwa badala ya kubadili matumizi.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Loema Peter, alisema fedha ambazo vikundi hivyo vinakopeshwa zinatokana na mapato ya ndani ikiwamo ushuru wanaotozwa kwenye biashara zao wanazozifanya.

Alisema kutokana na hali hiyo wananchi wanatakiwa kuacha kukwepa kutoa ushuru na kodi mbalimbali ambazo wanatozwa na serikali kwa maelezo kuwa sehemu ya malipo hayo ndio hizo zinarudi kwao kwa njia ya mikopo isiyokuwa na riba.

Peter alivitaka vikundi vinavyokopeshwa fedha hizo kuhakikisha vinairejesha kwa wakati ili kuepuka kuanza kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani kwa maelezo kuwa hilo sio lengo la serikali.

"Serikali haipendi kuwaletea polisi kwa ajili ya kuja kuwakamata, lakini ikitokea ndio hiyo huwa tunalazimika kufanya hivyo, mkurugenzi wetu huwa hapendi kabisa kufikia hatua hiyo hasa kwenu wanawake wenzake," alisema Peter.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Wilaya ya Rungwe, Mnkondo Bendera, alisema elimu inatakiwa zaidi kwa vikundi vya wanufaika ili wajue umuhimu wa kurejesha mikopo hiyo kwa wakati.

Alisema kuna uwezekano wananchi hao wanashindwa kurejesha mikopo hiyo kwa sababu hawana elimu ya kutosha ya ujasiriamali na hivyo wakikopeshwa wanafanyia shughuli zingine.

"Mtu ambaye ana elimu kama ana pikipiki mbili ataongeza ya tatu, lakini kwa yule ambaye hana elimu ya ujasiriamali, akipata mkopo huo anaweza akaongeza mke tofauti na lengo la serikali kwa hiyo toeni elimu," alisema Bendera.

Hata hivyo alivitaka vikundi vyote ambavyo vimeshanufaika na mikopo hiyo kurejesha kwa wakati ili vikopesheke zaidi na fedha hizo zinufaishe vikundi vingine.





# Makamu wa Pili wa Rais awataka Wazanzibari kujenga matumaini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah, amesema wananchi wa Zanzibar wanapaswa kujenga matumaini makubwa kwa serikali mpya itakayojizatiti kuwajibika ipasavyo katika kuwaletea maendeleo.

Alisema uwajibikaji huo utakaozingatia kutotoa nafasi kwa watendaji wenye tabia ya kukumbatia dhambi, ubadhirifu, uzembe pamoja na wizi ndio mfumo utakaotumiwa na serikali chini ya usimamizi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Akizungumza na wanahabari juzi nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, alisema viongozi watendaji wa umma pamoja na wananchi lazima waelewe kwamba kasi ya upatikanaji wa huduma muhimu za msingi za kustawisha jamii na kukua kwa uchumi itategemea ushirikiano mkubwa utakaohusisha serikali na wananchi.

Hemed alimshukuru Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi kwa kumwamini kumpa jukumu hilo zito ambalo ameahidi atalitekeleza kwa nguvu zake zote, ili kiu ya Wazanzibari ya kuiona falsaha ya yajayo yanafurahisha iweze kufikiwa katika muda mfupi.

Aliwathibitishia wananchi wote kwamba katika utekelezaji wake wa nafasi yake hatakuwa tayari kuona mtendaji aliyepewa dhamana ya kuwatumikia wananchi anazembea katika nafasi yake.



Askofu wa Kanisa Katoliki Zanzibar, Augustino Shao, akimpongeza mhitimu wa kidato cha nne wa shule hiyo, Shadya Lusekelo Lucas kwenye mahafali iliyofanyika juzi, Tomondo Zanzibar. **PICHA: MARTIN KABEMBA**.

# Usiri chanzo kesi za udhalilishaji kukwama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAHARAKATI wa kutetea haki za wanawake na watoto visiwani Zanzibar wameeleza kuwa usiri ni moja ya tatizo linalosababisha kesi nyingi za udhalilishaji kutofikia hukumu kwa kufutwa na nyingine kuondolewa mahakamani.

Ofisa ufuatiliaji na tathimini kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Mohamed Khatibu, alisema hayo wakati wa mkutano wa wadau na watetezi wa masuala ya udhalilishaji wa wanawake na watoto visiwani humo.

Khatib alisema kuwa kesi nyingi za udhalilishaji kwa wanawake na watoto kushindwa kufikia uamuzi kutokana na usiri na jamii bado haijawa tayari kuwafichukua wahalifu wa vitendo hivyo.

Hata hivyo, aliitaka jamii kuacha kupuuza vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto na wayachukulie kuwa ni sawa na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Alisema bado wapo baadhi ya watu wanayachukulia vitendo vya udhalilishaji kuwa kitu cha kawaida na kushindwa kuwalazimisha watoto wao kutoa taarifa sahihi wanapotendewa.

Alisema vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto ni miongoni mwa makosa ya jinai, hivyo huhitaji ushahidi wa kutosha ili kumtia hatiani mtuhumiwa na hatimaye aweze kuchukuliwa hatua.

Aliwaasa wadau hao kuwasisitiza watoto wao kutoa ushahidi wa kina na wenye kujitosheleza kuepuka adhabu mbadala ambayo shahidi wakati mwingine humkuta iwapo atakataa kutoa anapofika mahakamani. "Lazima wazazi mfahamu iwapo watoto wenu pia watakataa kutoa ushahidi sheria ipo wazi mtu huyo awekwe ndani kwa siku nane mpaka atakapokuwa tayari kutoa ushahidi," alisema.

Aliwaasa wadau hao kutoa elimu kwa wazazi na walezi kwa kuthamini jitihada zao na kukataa kuziacha njiani kesi za udhalilishaji huku wakifahamu kuwa kufanya hivyo ni kuvunja haki za watoto wao kwa kuwazaa.

Miongoni mwa wazazi ambao mtoto wake aliwahi kutoroshwa na kubakwa visiwani Zanzibar (jina tulihifadhi), alisema kama sio jitihada zake binafsi kesi yake isingeweza kufika mahakamani.

Alisema wakati kesi hiyo ikiwa kwenye hatua za awali, moja ya kituo cha polisi Mkoa wa Kusini Unguja, ilianza kufanyiwa ubabaishaji jambo ambalo alidai huenda ilikuwa njama dhidi yake kufutwa kwa kesi hiyo.

Hata hivyo, alisema hakurudi nyuma alikwenda kwa mkuu wa wilaya na ndipo kesi hiyo ilipoanza kufufuliwa na kupelekwa mahakamani na hatimaye mshtakiwa kufungwa miaka mitano jela.

Aliiomba jamii kuacha kurubuniwa kwa vitu vidogo pale watoto wao wanapofanyiwa vitendo hivyo kwa kuwa kufanya hivyo ni kudhalilisha zaidi utu wa mtoto.

Mwathirika mwingine wa vitendo hivyo ambaye mtoto wake alibakwa, alisema kesi ya mtoto wake ilimchukua muda mrefu zaidi kituo cha polisi jambo ambalo alidai lilikua na lengo la kumrudisha nyuma kufuatilia kesi hiyo.

Alisema baada ya kukutana na mazingira hayo alioamua kuomba msaada kutoka kwa mwanasheria jambo lilionekana kuwakasirisha maofisa wa polisi, lakini hakurudi nyuma.

Akieleza mafanikio yake alisema tayari jalada la kesi hiyo kwa sasa lipo ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka likisubiri kupangiwa siku ya kusomwa mahakamani.

Aliitaka jamii kutokata tamaa wanapokumbwa na kadhia hiyo badala yake wahakikishe wanafuatilia mpaka hatua ya mwisho.

# 'Hakuna maendeleo bila umoja'

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

ALIYEKUWA mgombea ubunge kupitia Chama cha NRA Jimbo la Ziwani Pemba, Abdullah Moh'd Said, amesema bila ya ushirikiano wa pamoja Zanzibar haiwezi kupata maendeleo.

Akizungumza jana na mwandishi wa habari huko Kisiwani Pemba, alieleza kuwa utawala uliopo madarakani umewekwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe kwa mazingira anayoyajua yeye na kuona kuwa unawafaa Watanzania.

Alisema kutokana na hilo Watanzania wa pande zote mbili hawanabudi kuunga mkono kwa dhati kabisa, ili viongozi walioko madarakani kuwatumikia wananchi wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

Alisema kuwa sio vyema kwa wananchi kukubali kushawishiwa kufanya vurugu zinazoweza kuhatarisha amani kwa kisingizio cha uchaguzi na kila mmoja anahitaji kuwa na amani na utulivu ili kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo za kujitafutia riziki za halali na kumuabudu Mungu.

"Utawala wowote ikiwa wa kifalme au huu tulionao wa kupatikana kwa kura hauwezi kupatikana iwapo Mwenyezi Mungu mwenyewe apende na amchague mmoja miongoni mwa wengi kuongoza wenzake hata kama kuna mambo yanafanyika tulioyaona na tuliokuwa hatukuyaona," alisema.

Aliwataka Watanzania kabla ya kuamua kuvunja amani, wakae na kutafakari ukubwa wa hasara na faida wanayoweza kuipata baada ya kufanya hivyo kwa maslahi ya wachache ya kidunia.

Said, alisema umoja wa taifa ni muhimu kuliko itikadi ya vyama vyao hivyo aliwasihi Wazanzibari na Watanzania kuwa makini katika suala zima la kudumisha umoja na upendo wao kama Watanzania na siasa isiwe chanzo cha mfarakano.

"Sio jambo la busara kwa Watanzania kuvipa nafasi vyama vyao vya siasa vikawa ni chanzo cha kutugawa kwa kuwa yanayopiganiwa ni maslahi ya kidunia tu, lakini udungu na umoja uliopo ni hazina kutoka kwa Mwenyezi Mungu," alisema.

Hata hivyo alisema uchaguzi umemalizika na watawala ndio wamepatikana pamoja na yote yaliojitokeza ni jambo la busara kukubaliana nayo kuijenga nchi yao kwa maslahi ya taifa na vizazi vyake.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA NA MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA IKO KAHAMA** MAJENGO VYUMBA VITATU INA MAJI NA UMEME, PLOT No 759, BLOCK "E", KIWANJA NI MEDIUM SIZE. MAWASILIANO ZAIDI; 0759359933/0713553819

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo **MJINI MOROGORO.**
Usimamizi wa mirathi No;332/2020
Ombi la **ABDULNASIR ALLY MJUNGU**,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MWAJUMA HAMISI MSANGI.**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **03/11/2020.**

Tarehe 03/11/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ALBERT ALEXANDER MGOYE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Mitsubishi Pajero yenye namba za usajili T 501 AGU.Chassis No.**CLO49VL5400681,** Engine **No.4D56CU6682.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi DOD/-DOD/RB/750434/2020.

## TANGAZO
### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RASHIDI SELEMANI SAID** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Mitsubishi Canter yenye namba za usajili T 739 DME. Chassis No. FE439E560628, Engine No. 4D34A27162. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DOM/RB/4730/2020.

## TANGAZO
### KUPOTEA KWA CHETI



**RAMADHANI ALLY RAMADHANI**
Amepotelewa na result slip na leaving certificate ya kidato cha nne vyenye **index namba** S4169/0337 kilichotolewa na shule ya secondary PENDAMOYO **mwaka 2019,yeyote** atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa DAR/CHA/RB/709634/2020

## TANGAZO
### KUPOTEA KWA CHETI



**ABASI MOHAMEDI AWESO**
Amepotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba** S 0340-00079 kilichotolewa na shule ya secondary POPATLAL mwaka **1999**,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa DAR/RB/786177/2020

## TANGAZO
### KUPOTEA KWA CHETI



AMEIR RAMADHANI HASSAN
Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba** S.403/0023/1989 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **MAKUNDUCHI**,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa DAR/KIG/RB/766254/2020

## TANGAZO
### KUPOTEA KWA CHETI



**MARTINE SYLVESTER MAGUTU**
Amepotelewa na vyeti,cha kidato cha nne **index No** S1470/0134 kilichotolewa na shule ya secondary KIARA mwaka 2009,kidato cha sita **index No S0134-0718** mwaka 2012 shule ya MOSHI secondary, cheti cha chuo na transcript BSC. Agricultural engineering chuo cha( SUA) SOKOINE UNIVERSITY,yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote ch polisi

Polisi taarifa MSV/RB/458/2020
Namba ya simu 0789349958.

## TANGAZO
### KUPOTEA KWA CHETI



**MARWA MAGEGU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba** S2558-0009 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SOMAGEDI SEKONDARI OCTOBA, 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No: 9910818026639.

## TANGAZO
### KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Charles Alexander Songo** ambaye ni msimamizi wa mirathi ya Marehemu **Alexander Songo** anatangaza kupotelewa na Ofa kiwanja **Namba 390 Kitalu "CC"** kilichopo eneo la Matanda manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu, au awasiliane na Charles Alexander Songo kwa simu namba **0756012598.**

RB Namba, RB/SHY/2020,
Control namba 9910819592366.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**THOMAS EVARIST MREMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA MITSUBISHI CANTER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 820 AUK**. Chassis namba **PE538B522795**. Engine 4D351XZF0306. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/MAG/RB/785686/2020.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

MIRATHI Na....... 70 YA MWAKA 2020
MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI
YA MAREHEMU **ELIKUNDA SAIBA MATERU**
MWOMBAJI/WAOMBAJI **MARRY SALALA**
TAARIFA YA KAWAIDA (KANUNI YA 75)

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 23 mwezi wa NOVEMBER / 2020.

Imewasilishwa Dar es salaam leo tarehe 3 mwezi wa NOVEMBER /2020

THE HIGH COURT OF TANZANIA
NAIBU MSAJILI
NAKALA KWA:

Nipashe

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Marais wapongeza ushindi wa Biden




Mmoja wa wafuasi wa Chama cha Democratic, akishangilia kushindwa kwa Donald Trump katika uchaguzi mkuu wa urais. **PICHA: ALLIANCE**

**AFRIKA,** Afrika

VIONGOZI kutoka nchi mbalimbali za Afrika wamempongeza Rais mteule wa Marekani, Joe Biden na makamu wake, Kamala Harris, kufuatia ushindi walioupata katika uchaguzi mkuu.

Biden aliibuka mshindi wa urais kwa kupata kura asilimia 50.7 dhidi ya mpinzani wake Donald Trump aliyepata asilimia 47.7.

**RAIS WA KENYA**

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta alisema: "Rafiki wa nchi yetu, ushindi wa Biden ulikuwa ishara ya Wamarekani kuamini uongozi wa makamu wa rais wa zamani".

Alisema Rais Biden ni rafiki wa nchi yetu ambaye ashawahi kututembelea na kusaidia kuimarisha ushirikiano madhubuti kati ya Kenya na Marekani.

Aliongeza kuwa ushindi wake unatoa fursa ya kuimarisha zaidi ushirikiano kati ya Kenya na Marekani.

Alisema Harris atakuwa kielelezo chema na atasaidia kuwapa motisha mamilioni ya wasichana wadogo kote duniani, kufikia ndoto yao ya kupata ufanisi maishani.

Rais Kenyatta pia alimshukuru Trump kwa utawala wake na kusema: "Tunamtakia kila la heri anapojiandaa kuondoka madarakani."

**RAIS WA UGANDA**

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni alimtumia salamu za pongezi Biden, kumkumbusha ushirikiano wa karibu wa nchi yake na Marekani.

Kwenye ukurasa wake wa Twitter, Rais Museveni aliandika: "Marekani na jamii yake ya watu weusi milioni 47.4, pamoja na idadi kubwa ya waumini wa Kikristo inatuunganisha kwa njia ya imani, hali ambayo kwa uhalisia ni maisha ya Waganda na Waafrika kwa jumla".

Aliongeza: "Marais wa zamani wa Marekani walitumia ushirikiano uliopo kwa kuweka sheria ya ukuaji na kuboresha nafasi ya biashara. Tunapongeza sera hiyo na kutumaini kuwa Biden ataudumisha."

**RAIS WA NAMIBIA**

Rais wa Namibia, Hage Geingob, alisema: "Wakati wa harakati zetu za kupigania uhuru, tulimfahamu kama seneta aliyepinga ubaguzi wa rangi Afrika Kusini na eneo lote hilo."

Aliongeza: "Natazamia kufanya kazi na Biden kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kibiashara ili kutoa mazingira huru duniani".

**RAIS WA LIBERIA**

Rais wa Liberia, George Weah, alisema: "Anachukuwa uongozi wa Marekani wakati nchi hiyo inakabiliwa na changamoto kubwa ya kiafya, hali ambayo pia inashuhudiwa kote duniani. Natoa wito kwa Wamarekani wote kusonga mbele pamoja kwa amani".

Aliongeza: "Kama washirika wa muda mrefu wa Marekani, Liberia iko tayari kufufua na kuimarisha uhusiano wetu wa biashara ya kihistoria".

**RAIS WA MISRI**

Rais wa Misri, Abdul Fattah al-Sisi, alisema: "Rais alisisitiza umuhimu wa kuchukua hatua ya pamoja ili kuimarisha uhusiano wa kibiashara kati ya Misri na Marekani, kwa maslahi ya nchi mbili rafiki na watu wake".

**RAIS WA ZIMBABWE**

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa alisema: "Zimbabwe inakutakia kila la heri katika uongozi wa watu Marekani. Natazamia kufanya kazi na wewe kuongeza ushirikiano kati ya nchi zetu mbili."

**RAIS WA GHANA**

Rais wa Ghana, Nana Akufo-Addo, alisema: "Ni matumaini yangu kwamba hatamu ya Rais mteule Biden uongozini italeta umoja, amani, maendeleo na ustawi kwa Wamarekani wote".

Aliongeza: "Nina matumaini kwamba uongozi wake, utaimarisha uhusiano ambao umekuwapo kwa miaka mingi kati ya Ghana na Marekani."

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, Rais wa Niger, Issoufou Mahamadou, Rais wa Senegal, Macky Sall, Rais wa Afrika Kusini Cyril, Ramaphosa na Rais wa Somalia, Mohamed Abdullahi Mohamed, nao walituma salamu za pongezi kupitia ukurasa wa Twitter.

"Natoa wito kwa Biden kutumia tajiriba yake kubwa kukabiliana na athari mbaya ya siasa ya utaifa katika masuala ya ulimwengu," kiongozi wa Nigeria alisema.

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, alitumai mkataba wa kibiashara utakaozipatia nchi za Afrika fursa ya kufikia soko la Marekani bila kutozwa kodi utatiwa saini upya.

Bi Harris alitajwa na Rais wa Kenya kama "trailblazer". Ameandikisha historia kama mwanamke wa kwanza, Mwafrika wa kwanza na Mmarekani mweusi kuwa makamu wa rais wa Marekani.

Baadhi ya viongozi wa bara la Afrika wamezungumzia rekodi ya bwana Biden na kukariri jinsi wanavyotazamia kufanya kazi na yeye. **BBC**

## Ethiopia yafanya mashambulizi ya angani

**ADDISABABA,** Ethiopia

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Aby Ahmed, ameimarisha operesheni ya kijeshi katika Jimbo la Kaskazini la Tigray, kwa kufanya mashambulizi ya anga ambayo ni sehemu ya kile alichokiita kuwa operesheni ya kuleta utiifu wa sheria.

Mashambulizi hayo yalikuwa sehemu ya operesheni ya kijeshi ya serikali kuu dhidi ya Jimbo la Tigray na kuongeza hofu ya kutokea vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi hiyo, ambayo ni ya pili kwa idadi kubwa ya watu barani Afrika.

Waziri Mkuu Ahmed alikataa kusikiliza miito kutoka Umoja wa Mataifa (UN) na washirika wake katika ukanda huo wa kumtaka akae kwenye mazungumzo na viongozi wa jimbo hilo la Tigray.

Jimbo hilo linakaliwa na jamii ya kabila lililowahi kuihodhi serikali kuu mjini Addis, kabla ya Abiy kuingia madarakani mwaka 2018.

Wiki iliyopita Abiy alianzisha operesheni ya kijeshi katika jimbo hilo akisema kwamba vikosi vitiifu kwa viongozi wa Tigray viliishambulia kambi ya jeshi la serikali kuu na kujaribu kupora vifaa.

Waziri Mkuu Abiy anawashutumu viongozi wa jimbo hilo kwa kuhujumu mageuzi yake ya kidemokrasia.

Ndege za kijeshi za serikali toka wakati huo zimekuwa zikishambulia maeneo ya jimbo hilo, ambalo linapakana na Sudan na Eritrea.

Juzi, wafanyakazi wa mashirika ya msaada walisema kwamba mapigano makali yalishuhudiwa katika maeneo mbalimbali ya jimbo hilo, kwamba watu wapatao sita waliuawa na wengine kadhaa kujeruhiwa.

Wakati huo huo, Abiy alimtangaza Mkuu wa Majeshi mpya, Mkuu wa Ujasusi na Kamishna Mkuu mpya wa Jeshi la Polisi, pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje.

Kutokana na uteuzi huo mpya, wachambuzi wa masuala ya kisiasa wamesema katika mabadiliko hayo, Abiy amewaweka kwenye ngazi za juu washirika wake, wakati mgogoro ukiwa unashika kasi. **DW**

# BARCA WASUBIRISHWA KWA NUNEZ HADI 2022




**LISBON,** Ureno

NYOTA wa Benfica, Darwin Nunez, atabaki kwa miamba hao wa Ureno angalau hadi mwaka 2022 wakati huu akihusishwa na Barcelona, kwa mujibu wa wakala wake, Edgardo Lasalvia.

Nunez alikuwa usajili ghali zaidi pale Benfica wakati aliposajiliwa kutoka Almeria kwa ada ya euro milioni 24 Septemba, mwaka huu na tayari ameshawavutia miamba wa LaLiga, Barca.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 21, alifungua akaunti ya mabao kwa kufunga 'hat-trick' kwenye michuano ya Ligi ya Europa mwezi uliopita, huku raia huyo wa Uruguay akiwa amefunga mabao matano kwenye mashindano yote msimu huu.

Juventus pia imekuwa ikihuishwa na kumwania Nunez na alipoulizwa kuhusu majaliwa ya straika huyo wa Benfica, Lasalvia aliiambia Sport: "Darwin atabaki Benfica angalau hadi mwaka 2022."

Kocha Mkuu wa Benfica, Jorge Jesus, alidokeza kwamba, Nunez ameziba pengo la Joao Felix ambaye aliuzwa kwa bei ghali zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Joao Felix aliondoka Benfica kwenda Atletico Madrid kwa ada ilyoweka rekodi klabuni hapo ya euro milioni 126.

# Zidane akubali kubeba lawama kipigo Real

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesema lawama zote abebeshwe yeye baada ya Real Madrid kuchapwa na Valencia kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, Jumapili.

Real Madrid iliruhusu mabao manne kwa mara ya kwanza kwenye mchezo wa Ligi Kuu chini ya Zidane.

Valencia waliibuka na ushindi huo wa 4-1 pale katika dimba la Mestalla baada ya Carlos Soler kuwa mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick ya penalti kwenye mchezo mmoja wa LaLiga katika karne ya 21.

Madrid ilionekana kuanza vizuri mchezo huo, baada ya kupata bao la uongozi lililofungwa na Karim Benzema, kabla ya Valencia inayonolewa na kocha Julen Lopetegui kupindua meza.

Zidane, ambaye alichukua nafasi ya Lopetegui, alikubali kwamba yeye ndiye wa kulaumiwa kwa kiwango kibovu kilichoonyeshwa na Madrid na kusema wanahitaji kufanyia kazi safu yao ya ulinzi.

"Penalti tatu na bao la kujifunga si sawa kabisa," alisema Zidane, ambaye kikosi chake kinashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi, kikipitwa pointi nne na vinara Real Sociedad.

"Makosa ni ya kwangu kwa sababu mimi ndio kocha na natakiwa kutafuta suluhisho. Siwezi kuelezea nini kilichotokea.

"Ilikuwa ni siku mbaya, hakuna cha kujitetea. Tunatakiwa kuimarisha safu yetu ya ulinzi kwa sasa."






# Dybala atemwa kikosini Argentina

**TURIN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Paulo Dybala, ameondolewa katika kikosi cha timu ya Taifa ya Argentina kwa mechi zinazokuja za kuwania kufuzu Kombe la Dunia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, aliingia dimbani akitokea benchi katika dakika 14 za mwisho, wakati Juve ikitoka sare ya kufungana bao 1-1 na Lazio, Jumapili na alionekana kutokuwa fiti.

Alikosa mechi mbili za kufuzu Kombe la Dunia za Argentina Oktoba, za ushindi dhidi ya Ecuador, Bolivia na sasa hatakuwapo kwenye mchezo dhidi ya Paraguay na Peru.

Argentina ilithibitisha katika taarifa yake ya Jumapili kwamba Dybala hatakuwapo kwenye kikosi hicho kwa sababu anatakiwa kupumzika kutokana na afya yake kutokuwa fiti.

Dybala ameichezea Juventus mechi sita kwenye mashindano yote msimu huu na amefunga bao moja wakati wakishinda 4-1 dhidi ya Ferencvaros kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mlinzi wa Ajax, Lisandro Lopez mwenye umri wa miaka 25, ameitwa na kocha Lionel Scaloni, ili kuziba nafasi yake, huku pia wakijumuishwa, Lionel Messi na Angel Di Maria.

HABARI MICHEZO

# Kimmich kurudi dimbani Januari

**MUNICH,** Ujerumani

JOSHUA Kimmich hajaumia sana na atarudi dimbani mwaka mpya baada ya kupata majeruhi kwenye mchezo wa Bayern Munich walioshinda 3-2 dhidi ya Borussia Dortmund.

Kulikuwa na hofu kwamba Kimmich ameumia sana na angeweza kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu, baada ya kugongwa goti na Erling Haaland kwenye mchezo wa Jumamosi wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Kiungo huyo alisaidiwa kutoka uwanjani, huku kocha Hansi Flick akisema kukosekana kwa Kimmich litakuwa pengo kubwa.

Lakini Bayern ilibainisha Jumapili kwamba, mchezaji huyo hakuumia kwa kiwango kikubwa na tayari ameshafanyiwa operesheni ndogo.

Mkurugenzi wa soka wa Bayern, Hasan Salihamidzic, aliongeza: "Tuna furaha Joshua pengine ataweza kuwa nasi tena kwa wiki chache zijazo.

"Tunampa sapoti kubwa wakati wote akiwa anaendelea kujiuguza na tutakuwa naye karibu wakati wote."





# GUARDIOLA AFURAHIA MSIMAMO CITY EPL

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesisitiza "ana furaha kubwa" kwa mwanzo huu wa msimu, ambao umeiacha timu yake nafasi ya 10 baada ya mechi saba za Ligi Kuu.

Gabriel Jesus alisawazisha bao la penalti la Mohamed Salah timu hiyo ikitoka sare ya kufungana 1-1 na Liverpool, pale kwenye Uwanja wa Etihad, Jumapili.

Alipoulizwa kama ana furaha na matokeo hayo baada ya mchezo huo, Guardiola alijibu: "Sana. Pengine nina furaha kuliko wakati mwingine wowote.

"Katika mechi 12 tumepoteza moja katika mashindano yote, dhidi ya Leicester.

"Nina furaha kubwa. Naona hali tofauti kila siku kwenye vyumba vya kubadilisha nguo, hivyo naamini mambo yatazidi kubadilika kila siku.

"Matumaini yangu wachezaji watarudi kutoka kwenye timu zao za taifa wakiwa salama bila majeraha."

Safu ya ushambuliaji ya City imekumbwa na majanga baada ya kuumia kwa Sergio Aguero na sasa akiwa amebaki na Jesus pekee.

Man City watarudi kwenye mchezo wa Ligi Kuu kwa kwenda kucheza na Tottenham Hotspur baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

# Fati afanyiwa upasuaji Barca

**BARCELONA,** Hispania

ANSU Fati atafanyiwa upasuaji wa mguu baada ya kuumia wakati Barcelona ikishinda 5-2 dhidi ya Real Betis.

Mshambuliaji huyo kinda alitolewa kipindi cha pili katika mchezo huo pale kwenye dimba la Camp Nou, Jumamosi na Barca baadaye ikathibitisha kwamba ameumia goti la mguu wa kushoto.

Fati jana Jumatatu alitarajiwa kufanyiwa upasuaji na Barca walisema watatoa taarifa zaidi kuhusu muda gani nyota huyo atakuwa nje ya dimba.

Taarifa ya klabu ilisomeka: "Mchezaji wa kikosi cha kwanza, Ansu Fati, atafanyiwa upasuaji baada ya kuumia goti la mguu wa kushoto. Atafanyiwa upasuaji chini ya usimamizi wa daktari wa klabu, Ramon Cugat.

"Baada ya matibabu yake kukamilika, tutatoa taarifa kamili kwamba kwa muda gani anaweza kuwa nje ya dimba."

Fati ndiye mchezaji anayeongoza kwa mabao katika kikosi cha Barca kwenye LaLiga msimu huu akiwa amefunga manne katika mechi saba, huku pia alifunga wakati wakishinda 5-1dhidi ya Ferencvaros kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kiwango chake kimekuwa cha kuvutia na amekuwa kikosi cha kwanza cha Barca chini ya kocha Ronald Koeman, ambaye alishuhudia kikosi chake kikishindwa kushinda mechi nne kwenye LaLiga kabla ya kuibuka na ushindi dhidi ya Betis.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PARTEY SASA AIPA MAJANGA ARSENAL

●●● Hatujui atakuwa nje kwa kipindi gani, tutamfanyia vipimo na kujua ameumia kwa kiwango...

**LONDON,** England

KIUNGO wa Arsenal, Thomas Partey, amezua hofu katika klabu hiyo kutokana na kutarajiwa kufanyiwa uchunguzi baada ya kuumia paja la mguu wa kushoto na hivyo kumweka shakani kuichezea Ghana mechi za kimataifa zinazokuja za kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika, Afcon.

Partey alitolewa kipindi cha pili wakati Arsenal wakichezea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Aston Villa kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumapili usiku.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alitengeneza pasi 36 katika kipindi cha kwanza na ambazo zilikuwa na usahihi kwa asilimia 80.6.

**Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, amethibitisha kwamba uamuzi wa kumtoa nje Partey, ambaye alijiunga na 'Washikabunduki' hao akitokea Atletico Madrid kipindi cha majira ya joto kilichopita, ulitokana na kuumia na si sababu za kiufundi.**

Partey alionekana akilishikilia paja lake la mguu wa kushoto kabla ya mapumziko na nafasi yake ikachukuliwa na Dani Ceballos.

Kiungo huyo, Partey alikuwa akitarajiwa kujiunga na kikosi cha Ghana wiki hii kwa ajili ya mchezo wa nyumbani na ugenini dhidi ya Sudan wa kufuzu kucheza michuano ya Afcon, unaotarajiwa kupigwa Alhamisi wiki hii na kurudiana Jumanne ya Novemba 17.

"Hatujui atakuwa nje kwa kipindi gani," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Leo (jana) tutamfanyia vipimo na kujua ameumia kwa kiwango gani. Ngoja tusubiri na tuone.

"Sina uhakika kama sasa atakwenda kwenye kikosi cha Ghana. Kama nilivyosema daktari ataangalia kiwango alichoumia, halafu tutaamua nini cha kufanya."

## ZISIKUPITE

### CONTE AMTAKA KANTE

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte, amebaki kuwa na nia ya kumsajili kiungo wa Ufaransa, N'Golo Kante, akitaka atue pale Inter Milan kipindi kijacho cha majira ya joto, lakini Real Madrid pia inamwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Canal, via Sun)***

### DEPAY HANA FURAHA LYON

WINGA wa zamani wa Manchester United, Memphis Depay, mwenye umri wa miaka 26, hana furaha pale Lyon na raia huyo wa Uholanzi bado anaifikiria Barcelona. ***(Sun)***

### MILAN WAMTAKA DALOT JUMLA

AC Milan inajaribu kuangalia kama Manchester United itakuwa tayari kumuuza kiungo wake wa kimataifa wa Ureno chini ya umri wa miaka 21, Diogo Dalot, baada ya kucheza kwa mkopo na klabu hiyo. ***(Tuttosport, via Inside Futbol)***

### WACHEZAJI, SOLSKJAER PAMOJA

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, bado anaungwa mkono na wachezaji wake, licha ya timu yake kutokuwa na kiwango cha kuvutia. ***(Mirror)***

### ARTETA KAMBAKISHA XHAKA

KIUNGO wa kimataifa wa Uswisi, Granit Xhaka, mwenye umri wa miaka 28, amekubali kwamba, "moyo wake uliondoka" kutoka Arsenal kabla ya Mikel Arteta kurudi na kuchukua mikoba ya kuinoa timu hiyo baada ya kuondoka kwa Unai Emery. ***(Mirror)***

### HOJBJERG KUIKOSA SPURS

KIUNGO wa Klabu ya Tottenham Hotspur, Pierre-Emile Hojbjerg, 25, ni miongoni mwa wachezaji wa Denmark watakaokosa mchezo ujao wa timu hiyo kutokana na kutakiwa kujitenga kwa sababu ya kubainika kuwa na virusi vya corona. ***(London Evening Standard)***

### MECHI YA LIVERPOOL HATIHATI

LIGI ya Mabingwa Ulaya ya Liverpool dhidi ya FC Midtjylland mwezi ujao inaweza isiwapo kwa sababu ya sheria mpya ya serikali ya Uingereza kuhusu kuruhusu wageni kuingia nchini humo kutoka Denmark. ***(Liverpool Echo)***

### TUCHEL AMSIFIA HERRERA

KOCHA wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel, amesema kiungo wa zamani wa Manchester United na Hispania, Ander Herrera "alikufa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo" kwa timu hiyo wakati akisifia kiwango cha nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 wakati wakishinda dhidi ya Rennes. ***(Mirror)***

### MOISE ASIFIWA PSG

STRAIKA wa Everton na Italia, Moise Kean, 20, ambaye anacheza kwa mkopo kule Paris St-Germain ameelezewa kama "mchezaji muhimu" na kocha Thomas Tuchel, baada ya mchezaji huyo kufunga mabao matano katika mechi tano. ***(Liverpool Echo)***

### SAHA AIFUNDA MAN UNITED

STRAIKA wa zamani wa Manchester United, Louis Saha, amesema 'Mashetani Wekundu' hao wanahitaji wachezaji wanne aina ya Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 26, ili kutoa changamoto kwenye mbio za kuwania taji. ***(Mirror)***

## HABARI MICHEZO

# Panga sasa laja Yanga

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Yanga unafikiria kupitisha panga kwa baadhi ya wachezaji wa timu hiyo ambao wameshindwa kuonyesha uwezo kwenye michezo mbalimbali ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea, imeelezwa.

Hatua hiyo ya uongozi inakuja baada ya kocha wa timu hiyo, Cedric Kaze kuweka wazi kuwa wapo baadhi ya wachezaji ambao hawaendani na kasi ya timu yake licha ya kuwapa nafasi ya kucheza kwenye baadhi ya michezo.

Baada ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya watani zao Simba, kocha Kaze alinukuliwa akisema wapo wachezaji ambao wanakaa benchi ila hawana uwezo sawa na wale wanaoanza kikosi cha kwanza, hivyo kumpa shida kuamua pindi mchezaji aliyeanza anapoumia au kukosekana kwenye mchezo.

Mmoja wa viongozi wa klabu hiyo, aliliambia Nipashe jana kuwa wanasubiri ripoti ya mwalimu (Kaze) kuona nini anachokitaka na uongozi utachukua hatua.

Kiongozi huyo ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Utendaji (hakutaka jina lake liwekwe hadharani), alisema uongozi nao umeona wapo wachezaji ambao ni 'mzigo' kwenye kikosi hicho hivyo wanasubiri maamuzi ya kocha wao.

"Mchezo dhidi ya Gwambina umeonyesha hali hiyo, wapo wachezaji wanapata nafasi, lakini hakuna wanachokitoa kwa timu... kocha anataka wachezaji ambao watakuwa na viwango sawa ili inapotokea mchezaji mmoja wa kikosi cha kwanza anakosekana basi awepo wa kuchukua nafasi yake bila shida," alisema mjumbe huyo.

Alipotafutwa Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Fredrick Mwakalebela (pichani chini), kulizungumzia suala hilo alisema suala la wachezaji na uwezo wao ni la benchi la ufundi, na kwamba uongozi utafuata kile ambacho kocha ataamua.

"Hakuna suala kama hilo, suala la wachezaji ni la kocha, yeye atatupa ripoti yake na sisi tutaifanyia kazi , kwa sasa timu imeelekeza nguvu kwenye michezo yake ya Ligi Kuu kama kutakuwa na chochote uongozi utatoa taarifa, suala la kuacha wachezaji nalisikia kwako," alisema Mwakalebela.

Wachezaji wa timu hiyo wamepewa mapumziko mafupi baada ya mchezo wao wa Jumamosi dhidi ya Simba na wanatarajia kurejea kwenye majukumu yao keshokutwa kujianda na mechi ijayo dhidi ya Namungo.

Katika kipindi hiki ambacho ligi imesimama kupisha michezo ya kimataifa ya timu za taifa, Yanga wamepanga kucheza michezo kadhaa ya kirafiki kujiweka sawa kabla ya ligi kuendelea Novemba 21.



# FRAGA NI PENGO SIMBA - MAGORI

**Na Adam Fungamwangwo**

MMOJA wa viongozi wa Simba, Crescentius Magori, amesema Simba iliathirika kwenye mechi ya watani wa jadi kutokana na kumkosa kiungo wake mkabaji, Gerson Fraga.

**Kauli hiyo imekuja baada ya kuishuhudia timu yao ikilazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi iliyopita.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Magori ambaye ni mshauri binafsi wa Mwekezaji wa Simba, Mohamed "Mo" Dewji, alisema kwa uchezaji ambao Yanga walikuwa wanacheza kwa kutumia zaidi nguvu, Fraga angeweza kabisa kusaidiana vema na Jonas Mkude kuwadhibiti.

"Pengo la Fraga ambaye anafanya shughuli pale katikati lilionekana. Kwa sababu sidhani kama wachezaji wa Yanga wangepita pale. Ilikuwa ni shida sana kukosekana kwake kwa sababu yeye amekuwa akiwasaidia na kuwalinda mabeki wa kati na pia uchezaji wa kutumia nguvu ungeenda sawa na wale wa Yanga, hivyo kungekuwa na shughuli," alisema Magori.

Fraga, aliumia dakika za mwanzo tu kwenye mechi kati ya timu ya Simba dhidi ya Biashara United na nafasi yake kuchukuliwa na Said Ndemla, mechi ikichezwa Septemba 20 na hadi leo hajarejea uwanjani.

Mbali na hayo, alisema pia kukosekana kwa Meddie Kagere na Chris Mugalu nako kulisababisha kupungua kwa mashambulizi ya Simba kwani ilikuwa inatumia straika mmoja tu, huku Yanga ikiweka mabeki wengi wa kati na viungo wa kukaba, pia wachezaji wengi wakiwa wanarudi nyuma kusaidia.

Magori amewasifu makocha wa pande zote mbili, Cedrick Kaze wa Yanga na Sven Vendenbroeck wa Simba kwa mbinu na mifumo waliotumia kiasi cha timu hizo kutawala kila moja kwenye kipindi kimoja tofauti, Yanga ikitawala kipindi cha kwanza na Simba ikitawala kipindi cha pili.

Wakati huo huo, kikosi cha Simba kinaingia kambini leo kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji utakaopigwa Novemba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven alisema wachezaji watakaoingia kambini ni wale ambao hawakuitwa kwenye vikosi vyao timu zao za taifa.

Simba ambayo inashika nafasi tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 20, nne nyuma ya Yanga inayoifukuzia Azam FC kileleni yenye alama 25, iliwapa siku mbili za mapumziko baada ya mechi hiyo ya Jumamosi.

**USHINDI...**



Wachezaji wa KVZ washerehekea kwa pamoja baada ya kukabidhiwa Ngao ya Jamii kwa kuifunga Mlandege FC mabao 2-1 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Mau A juzi. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# *Ngao ya Jamii yaifungua mdomo KVZ*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kufanikiwa kuanza msimu kwa kutwaa Ngao ya Jamii, timu ya KVZ, imesema taji hilo ni ishara ya wao kuanza kujipanga kuelekea kuubeba ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu wa 2020/21 unaotarajiwa kuanza rasmi Jumamosi wiki hii.

Katika mechi hiyo iliyokuwa maalum kwa ajili ya kukaribisha msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo ilipigwa Uwanja wa Mau A majira ya saa kumi alasiri, KVZ iliwachapa mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Mlandege FC kwa mabao 2-1.

Akizungumzia na Nipashe baada ya kuibuka na ushindi huo, Kocha Mkuu wa KVZ, Sheha Khamis, alisema wachezaji wake walistahili kushinda kwa kuwa walicheza vizuri na kwa umakini licha ya kupoteza nafasi nyingi katika kipindi cha kwanza.

"Ushindi huu wa Ngao ya Jamii ni ishara kuwa timu yake itaendelea kujipanga vizuri kuelekea Ligi Kuu Zanzibar Novemba 14, mwaka huu," alisema kocha huyo, ambaye timu yake ilipata nafasi hiyo ya kucheza na Mlandege kutokana na kutwaa ubingwa wa FA msimu uliomalizika.

Katika mchezo huo ambao ulihudhuriwa na mashabiki wengi huku timu zote zikitoshana nguvu kipindi cha kwanza, iliwachukua dakika 61 KVZ kuanza kuzifumania nyavu kupitia kwa Feisal Riambi, huku Maulid Maabad akihitimisha ushindi huo dakika 71.

Hata hivyo, Mlandege ilijiuliza zaidi na dakika ya 80 ilipata bao la kufutia machozi likifungwa na Fahad Mussa, lakini halikutosha kuweza kuwabeba taji hilo.

Kwa kutwaa taji hilo, mbali na kubeba ngao, KVZ ilitunukiwa medali sambamba na mshindi wa pili, Mlandege.

# Michezo

Jumanne Novemba 10, 2020

Nipashe




Partey sasa majanga Arsenal UKURASA 22

HUNIWEZI...



Beki wa Kati wa Arsenal, Gabriel dos Santos Magalhaes, akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Aston Villa wakati wakiangukia kichapo cha mabao 3-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yaonywa CAF

## ●●● Huku ikiwajua wapinzani wao Ligi ya Mabingwa Afrika, Tairone Santos atajwa, mabeki waonywa...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana usiku mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wakijua mpinzani wao watakayekutana naye katika hatua ya awali ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Afrika, benchi la ufundi la timu hiyo limeonywa kuhusu udhaifu mkubwa uliopo kwenye safu yao ya ulinzi, imeelezwa.

**Jana usiku droo ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ilifanyika jijini Cairo, Misri ambapo Simba inayoiwakilisha nchini kwenye Ligi ya Mabingwa na Namungo FC Kombe la Shirikisho, zimejua wapinzani wao watakaokutana nao hatua ya awali.**

Kutokana na kubanwa na ratiba ya Ligi Kuu Bara, huku ugumu wa kupata timu za nje kwa ajili ya kujipima nazo nguvu ukiongezeka kutokana na nchi nyingi kuwa kwenye karantini ya janga la corona, mbali na kusaka ubingwa, Simba na Namungo zimekuwa zikitumia mechi za Ligi Kuu kama sehemu ya maandalizi ya michuano hiyo ya CAF.

Hata hivyo, mechi ya watani wa jadi ambayo Simba ililazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga Jumamosi iliyopita, imeelezwa kuanika udhaifu mkubwa uliopo kwa mabeki wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara.

Mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, inaelezwa ndiyo mchezo wa kwanza kwenye ligi msimu huu kwa safu ya ulinzi ya Simba kukutana na washambuliaji wenye kasi na viungo wanaojua 'kugongana' ana kwa ana mabeki wa upinzani kwa muda wote wa mchezo.

Katika mechi hiyo iliyochezeshwa na waamuzi sita, beki wa Simba, Mkenya Joash Onyango, alishuhudiwa akishindwa kuhimili kasi ya winga wa Yanga, Tuisila Kisinda, kabla ya kumwangusha nje ya kidogo ya mstari wa 18, lakini kukosa umakini kwa mwamuzi wa kati Abdallah Mwinyimkuu, kulimfanya kuamuru ipigwe penalti iliyozamishwa nyavuni na Michael Sarpong dakika ya 31.

Lakini Onyango alifuta makosa yake kwa kuisawazishia Simba dakika ya 86, akiunganisha nyavuni mpira wa kona iliyopigwa na Luis Miquissone kutoka wingi wa kulia.

Akichambua udhaifu aliouona katika kikosi cha Simba baada ya mchezo huo wakati huu ikijiandaa kuelekea kwenye michuano ya kimataifa, aliyekuwa beki kisiki wa timu hiyo, George Masatu, amesema bado uongozi wa timu hiyo haujaweza kutatua tatizo lililokuwa likiwakabili msimu uliopita katika safu ya ulinzi.

Masatu alisema pamoja na ubora alionao Onyango aliyesajiliwa msimu huu baada ya kumaliza mkataba wake na Gor Mahia ya kwao, Kenya, bado hajawa suluhisho la udhaifu uliokuwapo katika safu ya ulinzi ya timu hiyo msimu uliopita.

"Mimi sijaona sababu ya kuachwa kwa beki Mbrazil Santos [Tairone Santos da Silva] na kusajiliwa kwa Onyango, ukiangalia bado uchezaji wao ni wa aina moja, na wote hawana kasi, hicho ndicho kilichomgharimu Onyango katika mechi dhidi ya Yanga," alisema Masatu.

"Santos alikuwa beki mzuri na anayetumia akili zaidi, lakini tatizo lilikuwa ni kasi kama ilivyo kwa Onyango, Simba ikikutana na washambuliaji wenye kasi muda wote kwenye michuano ya kimataifa mabeki hawataweza kuhimili."

Masatu aliwashauri wanaofanya usajili Simba kumulika mabeki waliokamilika kwa kila kitu kwa kuwa na uwezo wa kukaba vizuri, kutumia akili na wenye kasi, ili kuweza kufanya vizuri.

# Kaze: Niyonzima, Carlinhos sasa fiti

**Na Saada Akida**

HUKU akiwataka mashabiki wa Yanga na wachezaji wa timu hiyo kusahau matokeo ya sare dhidi ya watani zao Simba, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mrundi Cedric Kaze (pichani), amesema viungo wake waliokuwa majeruhi Haruna Niyonzima na Carlos Carlinhos, wamepona na wanaendelea na mazoezi.

Wachezaji hao hawakuwapo katika mechi zilizopita ikiwamo dhidi ya Simba ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam Jumamosi iliyopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema kwa sasa wameanza kufanya mazoezi na wanaweza kuwamo katika mipango yake kwenye mechi yao ijayo dhidi ya Namungo FC Novemba 22, mwaka huu, baada ya Kalenda ya Fifa kupita.



Alisema kuanzia jana wachezaji ambao hawajajiunga na timu zao za taifa, wataendelea na mazoezi, na kwa upande wake mechi dhidi ya Simba imeshapita na sasa wanaingia msituni kwa ajili ya maandalizi ya michezo mingine ya raundi ya 11 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Asante sana wananchi kwa sapoti yenu, tunarudi kazini leo (jana), kujiandaa na mechi yetu dhidi ya Namungo FC kuhakikisha tunafanya vizuri kwa kutafuta pointi muhimu, ligi imekuwa na ushindani mkubwa, hivyo hatuna muda wa kupoteza tunataka kuhakikisha makosa yaliyojitokeza tunayafanyia kazi mapema," alisema Kaze.

Yanga imetoa wachezaji saba Taifa Stars ambao wako kambini nchini Uturuki wakijianda na mechi ya kuwania kufuzu Afcon 2021 dhidi ya Tunisia, nyota hao ni Metacha Mnata, Bakari Mwamnyeto, Feisal Salum 'Fei Toto', Shaibu Abdallah 'Ninja', Farid Mussa na Ditram Nchimbi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >